**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**



**MHE. NASSOR AHMED MAZRUI**
**WAZIRI YA AFYA, ZANZIBAR**



**MHE. HASSAN KHAMIS HAFIDH**
**NAIBU WAZIRI WA AFYA, ZANZIBAR**



**DKT. HABIBA H. OMAR**
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA AFYA, ZANZIBAR**

# Sera ya Afya, 2011

## Dira:

*Kuwa na jamii yenye afya nzuri na uhakika wa kupata huduma za kinga na tiba.*

## Dhamira:

*Kuhakikisha kwamba Wazanzibari wote wanapata haki ya huduma bora za afya kwa misingi ya usawa kwa kuzingatia viwango na ubora vilivyowekwa kupitia afya ya msingi (Primary Health Care Approach).*

## Lengo Kuu la Sera:

*Kuimarisha huduma za afya za Kinga na Tiba na kuendeleza ustawi wa watu wa Zanzibar kwa kutilia mkazo zaidi wanawake, watoto pamoja na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu.*

**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# WIZARA YA AFYA ZANZIBAR

## HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA
## MHE. NASSOR AHMED MAZRUI
## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2024/2025

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

***Juni, 2024***

# YALIYOMO


***Mada*** ***Ukurasa***

MCHANGANUO WA VIFUPISHO .......................................................................... iii

A. UTANGULIZI ...................................................................................................... 1

B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA ............................................ 4

C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 ............................................................................................ 5

*MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ........................ 5*

*MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA FEDHA 2023/2024 .............................. 9*

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101) .......................................... 12

*HUDUMA ZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI, HOMA YA INI, KIFUA KIKUU NA UKOMA ............................................................................................................. 13*

*HUDUMA ZA KUMALIZA MALARIA ZANZIBAR ................................................ 17*

*HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO ............................................ 20*

*HUDUMA ZA MARADHI YASIYOAMBUKIZA ...................................................... 23*

*HUDUMA YA UFUATILIAJI WA MIENENDO YA MARADHI ................................. 24*

*HUDUMA ZA MARADHI YASIYOPEWA KIPAUMBELE ....................................... 25*

*HUDUMA ZA MSINGI ZA MATIBABU YA MACHO ............................................ 26*

*HUDUMA YA UTOAJI WA ELIMU YA AFYA NA URATIBU WA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII .................................................................................................. 26*

*HUDUMA ZA AFYA YA MAZINGIRA .................................................................. 29*

*HUDUMA ZA AFYA MIPAKANI (BANDARINI NA VIWANJA VYA NDEGE) ........... 30*

*HUDUMA YA AFYA YA WAFANYAKAZI ............................................................. 31*

*HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI YA AKILI ........................................................... 32*

UTEKELEZAJI WA BODI NA MABARAZA YA TAALUMA ZA AFYA ............................ 33

*BARAZA LA TAALUMA ZA AFYA YA JAMII NA MAZINGIRA ............................... 33*

PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102) ....................................................... 34

*HUDUMA ZA UCHUNGUZI ................................................................................ 36*

*HUDUMA ZA USHIRIKIANO WA AFYA KIMATAIFA ........................................... 36*

*HUDUMA ZA DAMU SALAMA ........................................................................... 37*

*HUDUMA ZA MKONO KWA MKONO (ONE STOP CENTRE) ............................. 38*

*HUDUMA ZA BODI NA MABARAZA YA TAALUMA ZA AFYA ............................. 38*

*BODI YA USHAURI YA HOSPITALI BINAFSI ...................................................... 38*

*BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA ZA TIBA ........................................... 40*

*BARAZA LA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA ..................................................... 40*

*BARAZA LA MADAKTARI ................................................................................... 41*

*BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA ............................................................. 42*

*HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA ................................................................. 42*

HUDUMA YA UPATIKANAJI, UHIFADHI, USAMBAZAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA ... 44
*OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI ...................................................... 44*
*WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA ............................................................ 45*
PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI (SH030202) .......................... 47
HUDUMA ZA WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ........................... 47
*WAKALA WA MKEMIA MKUU WA SERIKALI .................................................. 47*
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0103) ....................... 50
PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI (SH010301) .................. 51
NGUVUKAZI YA SEKTA YA AFYA .................................................................... 51
*USIMAMIZI WA SHERIA .................................................................................. 52*
*HUDUMA ZA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA .......................... 53*
*HUDUMA ZA AFYA KIDIJITALI ......................................................................... 54*
PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI (SH010302) ...................... 56
*MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZHSF) ......................................... 59*
*TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZA BINAADAMU – (ZAHRI) ................................ 62*
*PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA WIZARA YA AFYA PEMBA (SH010303).. 65*
*PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (FUNGU H02) .............................. 66*
*PROGRAMU NDOGO YA UCHUNGUZI NA MATIBABU (SH0201) ....................... 68*
*PROGRAMU NDOGO YA UONGOZI NA UTAWALA (SH0202) ............................ 70*
*UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ..................................................... 71*
D. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA HATUA ZA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA .................................................................. 73
HATUA ZA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA .............................. 74
E. MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ............................................................................... 75
PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA .................................................. 75
PROGRAMU YA TIBA ...................................................................................... 76
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PHO103) ......... 78
PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (HO2) ........................................ 79
F. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ............................................................................... 81
G. SHUKRANI ............................................................................................ 83
H. HITIMISHO ............................................................................................ 85
MAOMBI YA FEDHA KWA UTEKELEZAJI WA KAZI ZILIZOPANGWA KWA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ....................................... 85

# MAELEZO YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AMREF | - | Africa Medical Research Foundation |
| ARV | - | Anti-Retroviral Virus |
| BADEA | - | Arab Bank for Economic Development in Africa |
| BOQ | - | Bill of Quantities |
| CT scan | - | Computed Tomography |
| CBM | - | Christian Blind Mission |
| CDC | - | Centre for Disease Control and Prevention |
| CPAP | - | Continuous Positive Airway Pressure |
| DNA-PCR | - | Deoxyribonucleic acid - Polymerase Chain Reaction |
| DR6000 | - | DR6000 UV VIS Spectrophotometer with RFID Technology |
| DFID | - | Department for International Development |
| EMR | - | Electronic Medical Records |
| EAC | - | East African Community |
| GCP | - | Google Cloud Platform Services |
| GFATM | - | Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria |
| GIZ | - | German Agency for International Cooperation |
| HPV2 | - | Human papillomavirus types 2 (HPV-2) |
| HIPZ | - | Health Improvement Project Zanzibar |
| IHI | - | Ifakara Health Institute |
| JKCI | - | Jakaya Kikwete Cardiac Institute |
| JICA | - | Japan International Cooperation Agency |
| JHPU | - | Jandy JHP & JHPU Pump Parts |
| KVZ | - | Kikosi cha Valentia Zanzibar |
| LCMS | - | Lutheran Church – Missouri Synod |
| KFD | - | Kyasanur forest disease |
| KMKM | - | Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar |
| MOI | - | Muhimbili Orthopaedic Institute (MOI) |
| MS | - | Multiple sclerosis |
| MDH | - | Management and Development for Health (MDH) |
| MBLW | - | Memba wa Baraza La Wawakilishi |
| MIOT | - | Madras Institute of Orthopedics’ and Traumatology |
| MRI | - | Magnetic Resonance Imaging |
| MP-AES | - | Microwave Plasma Atomic Emission Spectoscopy |

| | | |
|---|---|---|
| MNAP | - | Multisectoral Nutrition Action Plan |
| NHIF | - | National Health Insurance Fund |
| PEPFAR | - | The U.S. President's Emergency Plan for AIDS Relief |
| PENTA | - | Pentavalent vaccine |
| PMI | - | President's Malaria Initiatives |
| PPH | - | Postpartum Hemorrhage |
| PDB | - | Presidental Delivery Bureau |
| SMT | - | Surface-Mount Technology |
| SFD | - | Sorsby Fundus Dystrophy |
| SMZ | - | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TASAF | - | Tanzania Social Action Fund |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| THPS | - | Tanzania Health Promotion Support |
| UNFPA | - | United Nations Population Fund |
| UNAIDS | - | United Nations Programme on HIV/AIDS |
| UNDP | - | United Nations Development Program |
| USAID | - | United States Agency for International Development |
| U.A.E | - | United Arab Emirates |
| UNICEF | - | United Nations International Children Fund |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UAT | - | User Acceptance Testing |
| UVKO-19 | - | Ugonjwa wa Virusi vya Korona - 19 |
| VVU | - | Virusi Vya UKIMWI |
| WHO | - | World Health Organization |
| ZCTV | - | Zanzibar Cable Television |
| ZBC | - | Zanzibar Broadcasting Cooperation Television |
| ZanLIS | - | Zanzibar Laboratory Information System |
| ZADEP | - | Zanzibar Development Plan |
| ZAHRI | - | Zanzibar Health Research Institute |
| ZSSF | - | Zanzibar Social Security Fund |
| ZHSF | - | Zanzibar Health Services Fund |
| ZFDA | - | Zanzibar Food and Drug Agency |
| ZOP | - | Zanzibar Outreach Program |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu likae kama kamati ya matumizi ili iweze kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa leo kwa mara nyengine mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/25. Aidha, kipekee naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu katika hali ya amani na utulivu pamoja na kujenga imani kwangu katika kuisimamia sekta muhimu inayogusa maisha ya kila mwananchi. Pia nichukue fursa hii kumpa pole Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kufiwa na Baba yake mzazi marehemu **Ali Hassan Mwinyi**, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema **Peponi Amin**.

3. **Mheshimiwa Spika,** hatuna budi kumpongeza na kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais Wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kufanya mabadiliko makubwa kwenye sekta zote nchini ikiwemo sekta ya afya kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi, kwa ujenzi wa hospitali za Wilaya na Mkoa na kuwekwa dawa na vifaa tiba vya kisasa na vinavyokwenda na wakati kwa lengo la kutoa huduma bora za afya.

4. **Mheshimiwa Spika,** vile vile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Othman Masoud Othman** Makamo wa Kwanza wa Rais na **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah** Makamo wa Pili wa Rais kwa maelekezo yao wanayonipatia mara kwa mara ili kuhakikisha huduma za afya zinaimarika kuanzia ngazi ya jamii hadi hospitali za rufaa. Aidha nachukua fursa hii kumshukuru **Mama Maryam Mwinyi** na Taasisi yake ya Zanzibar Maisha Bora Foundation kwa mashirikiano makubwa katika kuimarisha sekta ya Afya nchini ikiwemo kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto na kuimarisha huduma za lishe kwa wananchi. Vilevile, nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi **Mhandisi Zena Ahmed Said** kwa ushauri na maelekezo anayotupatia katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za wizara.

5. **Mheshimiwa Spika,** Nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili kwa umakini kabisa. Pia nawapongeza Naibu Spika, **Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wa Baraza** na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa namna wanavyotoa hoja na michango inayopelekea kuleta ufanisi na uwajibikaji wa watendaji wa taasisi mbali mbali na kurahisisha maendeleo. Napenda kukuhakikishia kuwa uongozi wa Wizara ya Afya utaendelea kusimamia utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo, ushauri na maelekezo yanayotolewa na Baraza lako tukufu namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima, busara na umakini.

6. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii inayoongozwa na **Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani** Mwakilishi wa Viti Maalum, kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa yenye lengo la kuimarisha huduma za afya nchini hususan wakati wanapofanya ziara katika taasisi za Wizara. Ninawaahidi waheshimiwa wajumbe kuwa Wizara yangu itaendelea kuzingatia ushauri na mapendekezo yenu katika kutekeleza majukumu yetu kwa wananchi.

7. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya shukurani hizo, napenda kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha **2023/2024**, Mpango wa

Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza malengo na vipaumbele vya sekta kwa mwaka **2024/25**.

## MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya ina jukumu la kuimarisha huduma za afya za kinga na tiba na kuendeleza ustawi wa watu wa Zanzibar kwa kutilia mkazo zaidi wanawake, watoto pamoja na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu. Dhamira hii itafikiwa kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zinazotolewa katika hali ya ubora, usawa na ufanisi kwa watu wote wa Zanzibar.

## B. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024.

### *MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024*

9. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Afya, (**Fungu H01**) ilikadiriwa kutumia Shilingi **189,379,436,000/=** zikijumuisha Shilingi **60,013,800,000/=** kwa ajili ya mishahara; Shilingi **58,627,086,000/=** kwa kazi za kawaida; shillingi **5,062,598,460/=** kwa Ruzuku na Shilingi **65,675,951,540/=** kwa kazi za Maendeleo. Kati ya hizo Shilingi **53,050,000,000/=** kutoka serikalini na Shilingi **12,625,951,540/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

10. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja (**Fungu H02**) ilikadiriwa kutumia shilling **49,772,000,000/=** zikihusisha Shilingi **24,372,400,000/=** kwa ajili ya mishahara na Shilingi **14,274,400,000/=** kwa kazi za uendeshaji wa Hospitali na Shilingi **11,125,200,000/=** kwa Miradi ya maendeleo. Kati ya hizo Shilingi **1,125,200,000/=** kutoka Serikalini na Shilingi **10,000,000,000/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

11. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2024 Wizara ya Afya, (Fungu H01) ilikadiriwa kutumia Shilingi **142,481,995,150/=** zikijumuisha Shilingi **45,010,350,000/=** kwa ajili ya mishahara; Shilingi

**43,970,314,500/=** kwa kazi za kawaida; shillingi **3,796,948,845/=** Ruzuku na Shilingi na **49,704,381,805/=** kwa kazi za Maendeleo. Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) ilikadiriwa kutumia shillingi **37,048,200,000/=** zikihusisha Shilingi **18,279,300,000/=** kwa ajili ya mishahara, Shilingi **10,425,000,000/=** kwa kazi za uendeshaji wa Hospitali na Shilingi **8,343,900,000/=** kwa Miradi ya maendeleo ambapo Shilingi **843,900,000/=** kutoka Serikalini na Shilingi **7,500,000,000/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara ya Afya (Fungu **H01**) iliingiziwa Shilingi **112,410,274,745.58/=** sawa na asilimia **78.8** ya fedha zilizotengwa jumla ya Shilingi **142,481,995,150/=** kwa robo tatu zikiwemo fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kati ya hizo Shilingi **50,739,546,591/=** sawa na asilimia **112.7** kwa ajili ya mishahara, Shilingi **30,734,835,084.71/=** sawa na asilimia **69.9** kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi **3,994,873,973/=** sawa na asilimia **105.2** kwa ajili ya Ruzuku**.** Aidha, Shilingi **26,941,019,096.87/=** sawa na asilimia **54.2** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya hizo Shilingi **22,282,784,759/=** kutoka Serikalini, na Shilingi **4,658,234,337.87/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

13. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Hospitali ya Mnazi Mmoja (**Fungu H02**) iliingiziwa Shillingi **28,639,226,773/=** sawa na asilimia **77.3** zikihusisha Shilingi **16,453,275,382/=**

kwa ajili ya mishahara, Shilingi **11,140,000,000/=** kwa kazi za uendeshaji wa Hospitali na Shilingi **2,016,856,391/=** kwa Miradi ya maendeleo ambapo Shilingi **1,045,951,390/=** zimetoka Serikalini na Shilingi **970,905,000/**= kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo unapatikana katika **kiambatisho nambari 1a na 1b.**

14. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Afya (**Fungu H01**) ilikadiriwa kukusanya Shilingi **5,751,881,000/=**, ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ilikadiriwa kukusanya Shilingi **4,313,910,750/=**. Hadi kufikia Machi 2024, makusanyo yamefikia Shilingi **2,154,848,357/=** sawa na asilimia **49.9** ya makadirio ya robo tatu ya mwaka. **Kiambatisho nambari 1c kinafafanua**.

15. **Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Mnazi Mmoja (**Fungu H02**) kwa mwaka fedha 2023/2024 ilikadiriwa kukusanya shillingi **1,348,585,369/=.** Aidha kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi **1,012,535,500/=** kupitia vyanzo vya malipo ya Huduma za Afya ikiwemo, huduma za Haraka (Fast Track), huduma za Bima na malipo ya wanafunzi wa kigeni. Hadi kufikia Machi, 2024 Hospitali ya Mnazi Mmoja imekusanya jumla ya Shilingi **505,714,452.85/=** sawa na asilimia **49.9**. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana kwenye **kiambatanisho nambari 1d**.

16. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Sera ya Afya ya mwaka 2011 ambayo imeshafanyiwa mapitio mwaka 2024, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025, Mpango Mkakati wa Nne wa Sekta ya Afya (Health Sector Strategic Plan IV 2021/22-2024/25), Maagizo ya Serikali kupitia Taasisi ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa shughuli Serikalini (Presidential Delivery Bureau) pamoja na makubaliano ya Kikanda na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/24 Wizara kupitia Taasisi, Idara, Vitengo, Programu na Washirika wa maendeleo ilipanga kutekeleza shughuli mbali mbali zenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

    i. Huduma za afya ya Uzazi, Lishe, Mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga;
    ii. Miundombinu ya kutolea huduma za Afya katika ngazi zote;
    iii. Upatikanaji wa Dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote za utoaji wa huduma;
    iv. Mifumo ya kugharamia huduma za afya ikiwemo Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar;
    v. Ubora na kuongeza idadi ya rasilimali watu, hususan katika kada muhimu;

vi. Kinga na kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya, maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza;
vii. Mifumo ya Tehama na matumizi ya taarifa za afya katika kuboresha huduma.; na
viii. Huduma za tiba kwa mashirikiano na sekta binafsi (Out-sourcing).

***MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA FEDHA 2023/ 2024***

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa nimshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kuendelea kuipa kipaumbele sekta ya afya kwa kutoa miongozo na maelekezo mbalimbali pamoja na kufanya uwekezaji mkubwa ili kuimarisha huduma za afya kwa wananchi;

Naomba kutambua mambo **18** makubwa yaliyotekelezwa na Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** katika kipindi cha uongozi wake kama ifuatavyo: -

i. Kuendeleza ujenzi wa nyumba za makaazi ya Wafanyakazi kwenye Hospitali za Wilaya na Mkoa kutoka hospitali nne (**4**) hadi tisa (**9**);
ii. Kuanza kutoa huduma za matibabu kwenye hospitali mpya za wilaya na mikoa;
iii. Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za dawa muhimu katika vituo vya afya na hospitali, upatikanaji wa dawa

hizo umeongezeka kufikia asilimia **90** kwa hospitali za Wilaya na kwa upande wa vituo vya afya umefikia asilimia **73** ukilinganisha na asilimia **63** kwa mwaka 2022/2023;

iv. Kuimarika kwa upatikanaji na usambazaji wa dawa ambapo utaratibu wa sasa unafanyika kila mwezi kwa vituo vyote;

v. Kupitishwa Sheria ya Bohari Kuu ya Dawa kuwa Wakala;

vi. Kuanza kutoa huduma kwa wanachama wa Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF);

vii. Ongezeko la kiwango cha utoaji wa chanjo za watoto chini ya miaka mitano kutoka asilimia **84** kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia asilimia **95** kwa mwaka 2023/2024;

viii. Kuongezeka kwa idadi ya vitanda vya kulaza wagonjwa katika hospitali za Serikali kutoka vitanda **1,445** mwaka 2022 hadi vitanda **2,645** kwa mwaka 2024;

ix. Kuimarika kwa huduma za wagonjwa mahututi kwa kuongezeka vyumba ya kutoa huduma hiyo kutoka chumba kimoja **(1)** katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa mwaka 2022 hadi kufikia vyumba **14** katika Hospitali za Wilaya na Mkoa kwa mwaka 2024;

x. Kuongezeka kwa idadi ya vitanda kwa ajili ya wagonjwa mahututi katika hospitali za Serikali kutoka vitanda vinane (**8**) mwaka 2022 hadi vitanda **84** kwa mwaka 2024;

xi. Kuongezeka kwa vyumba vya upasuaji (Theatres) kutoka vyumba **11** ambapo vyumba vya upasuaji viwili (**2)** tu vilikua kwa ajili ya kina mama wenye mahitaji ya

kujifungua kwa njia ya upasuaji hadi kufikia vyumba **35** ikiwemo vyumba **13** maalumu kwa ajili ya kinamama wanaolazimika kujifungua kwa njia ya upasuaji;

xii. Kuongezeka kwa idadi ya vitanda vya mama wajawazito kabla ya kujifungua, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua katika hospitali za Serikali kutoka vitanda **229** kwa mwaka 2022 hadi vitanda **411** Kwa mwaka 2024;

xiii. Kuongezeka kwa hospitali zenye uwezo wa kutoa huduma za watoto njiti (Neonatal ICU) kutoka hospitali mbili (**2**) kwa mwaka 2022 hadi hospitali **13** kwa mwaka 2024;

xiv. Kuongezeka kwa hospitali zinazotoa huduma za tiba za dharura kutoka hospitali mbili (**2**) 2022 hadi kufikia hospitali **14** kwa mwaka 2024;

xv. Kuimarika kwa huduma za uchunguzi kutoka mwaka 2021/2022 hadi kufikia 2023/2024 kwa kuongezeka kwa vifaa vya kisasa vya uchunguzi kutoka MRI moja (**1**) hadi mbili (**2)**, CT-Scan moja (**1)** hadi tatu (**3)**, Digital X-ray tatu (**3)** hadi **15** na Ultrasound **10** hadi **34**;

xvi. Kuanza kazi kwa maabara mpya ya kisasa ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar;

xvii. Kurasimishwa kwa kada ya wahudumu ya afya ya jamii na kuanzishwa Kitengo maalumu cha kusimamia shughuli za watoa huduma za afya wa ngazi ya jamii; na

xviii. Kuanzishwa kwa kituo cha mawasiliano ya magonjwa ya dharura na miripuko (Zanzibar Afya Call Centre).

19. **Mheshimiwa Spika,** maelezo zaidi ya mafanikio hayo na mengineyo yanaelezwa kwa kina katika utekelezaji wa shughuli zilizofanyika kupitia huduma zinazotolewa katika kila programu husika kama ifuatavyo:

## PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA (PH0101)

20. **Mheshimiwa Spika**, jukumu la Programu hii ni kuhakikisha jamii inapata huduma bora za kinga pamoja na kuongeza uelewa kwa njia mbalimbali za kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Programu ya Kinga na Elimu ya Afya ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

    i. Kuendelea kudhibiti maambukizi ya VVU kwa kutoa huduma za ushauri nasaha, upimaji na matibabu;

    ii. Kuendelea kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini;

    iii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto;

    iv. Kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kumaliza Malaria Zanzibar;

    v. Kuimarisha huduma za Afya ya mipakani (Bandari na Viwanja vya Ndege);

    vi. Kuendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa maradhi ya macho katika skuli, vituo vya afya na hospitali;

    vii. Kuendelea na mikakati ya kupambana na Maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza;

viii. Kuendelea na mkakati wa kubadilisha tabia hatarishi zinazochangia kuenea kwa maradhi yasiopewa kipaumbele hapa Zanzibar;

ix. Kuimarisha afya ya jamii na mazingira;

x. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali ili kuimarisha huduma za afya katika kupambana na maradhi;

xi. Kuimarisha program za uhamasishaji na kutoa elimu ya afya katika ngazi zote; na

xii. Kuendelea kuimarisha kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya.

21. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara ya Afya kupitia fungu (PH0101) ilitenga jumla ya Shilingi **19,443,168,390/=** Kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa kupitia Programu ya Kinga na Elimu ya Afya ambapo hadi kufikia Machi 2024 kiasi cha Shilingi **18,159,392,286/=** zilitumika sawa na asilimia **93** ya fedha zilizotengwa katika programu hii. Utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa katika programu hii unaelezwa kupitia huduma mbali mbali zilizotolewa kama ifuatavyo:

**HUDUMA ZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI, HOMA YA INI, KIFUA KIKUU NA UKOMA.**

22. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya fedha iliyotengwa ni Shilingi **3,291,273,545.70/=** (Serikalini **397,912,843/=** na Washirika wa Maendeleo **2,893,360,702.70/=**). Hadi

kufikia Machi 2024, Jumla ya Shilingi **1,486,543,267/=** (Serikali **125,000,000/=** na Washirika wa Maendeleo **1,361,543,267/=**) sawa na asilimia **45.17** ya fedha zote ziliingizwa.

23. **Mheshimiwa Spika**, Katika kupambana na maambukizi ya VVU Wizara imedhamiria kutokomeza ugonjwa huu ifikapo 2030. Hadi kufikia machi 2024 jumla ya watu **65,643** (Wanaume **29,990** na Wanawake **35,653**) walipatiwa huduma za ushauri nasaha na uchunguzi wa VVU, kati ya hao **572** (**0.8%**) waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU ambao watu **519** Unguja (wanawake **353** na wanaume **166**) na Pemba **53** (wanawake **32** na wanaume **21**). Huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU kwa mwaka 2023/24 umeshuka ikilinganishwa na upimaji wa VVU kwa mwaka 2022/23 ambapo jumla ya watu **93,912** walipimwa VVU, kati ya hao, watu **659** (**416** wanawake na **243** wanaume) waligundulika na maambukizi ya VVU sawa na asilimia **0.7**.

24. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, jumla ya kinamama wajawazito **51,480** walihudhuria kliniki wakati wa ujauzito, kati ya hao, **46,430** walipimwa VVU sawa na asilimia **90** ikilinganishwa na asilimia **96** ya upimaji wa VVU kwa mwaka 2022/23. Aidha, jumla ya wajawazito **58** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU ambapo wajawazito wote hao waliweza kuunganishwa kliniki za huduma na tiba kwa wanaoishi na VVU pamoja na kuanzishiwa dawa za kupunguza

makali ya VVU. Vilevile, jumla ya watoto **347** waliozaliwa na mama wanaoishi na VVU wamepimwa VVU kwa kutumia mashine ya DNA-PCR ambapo jumla ya watoto **6** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU sawa na asilimia **1.7** ikilinganishwa watoto waliopimwa mwaka 2022/2023 ambapo watoto **212** walipimwa VVU na **3** kugundulika na maambukizi ya VVU sawa na asilimia **1.4**.

**25. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kwa kutoa huduma mjumuisho za kuzuia maambukizi ya Kaswende na Virusi vya Homa ya Ini aina B. Jumla ya wajawazito **24,401** wamepimwa kaswende. Hadi kufikia Machi 2024 kati ya wajawazito **51,480** waliohudhuria kliniki sawa na asilimia **47** ikilinganishwa na asilimia **59.2** walipimwa kaswende mwaka 2022/23, kati ya mama hao **42** waligundulika kuwa na maambukizi na wote wamepatiwa matibabu ya Kaswende. Katika kupambana na mambukizi ya homa ya Ini B jumla ya wajawazito **19,329** wamepimwa kipimo cha Homa ya Ini B, na mama **108** sawa na asilimia **0.5** walikutwa na maambukizi na tayari wameunganishwa kwenye huduma za matibabu ya homa ya ini B.

**26. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024, Jumla ya watu **18,922** (wanaume **8,676** na wanawake **10,246**) walipimwa virusi vya homa ya Ini B, kati ya hao, watu **1,302** (**710** wanaume na **592** wanawake) sawa na asilimia **6.8** wamegundulika kuwa na maambukizi ya virusi

vya homa ya Ini B. Jumla ya wateja wapya wenye maambukizi ya virusi vya homa ya Ini B **473** (**214** wanaume na wanawake **259**) wamesajiliwa katika kliniki za homa ya Ini Unguja na Pemba.

27. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa huduma ya homa ya Ini C, Jumla ya watu **18,014** (**8,511** wanaume na wanawake **9,503**) walipimwa kuangalia virusi vya homa ya Ini C na watu **184** (wanaume **152** na wanawake **32**) sawa na asilimia **1.0** wamegundilika kuwa na maambukizi ya vimelea vya homa ya Ini C ikilinganishwa na mwaka 2022/2023 ambapo idadi ya wagonjwa waliogundulika walikuwa **81** (**67** wanaume na **14** wanawake) Unguja na Pemba.

28. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024 Jumla ya wateja **8,691** (**2,686** wanaume na **6,005** wanawake) wanaoishi na VVU wanendelea kupatiwa huduma kwenye kliniki **14** (**10** Unguja, **4** Pemba) za huduma na tiba kwa wanaoishi na VVU. Kati ya hao **8,561**(**2,646** wanaume na **5,915** wanawake) sawa na asilimia **98.5** wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs). Aidha, kwa kipindi Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya wateja wapya wanaoishi na VVU waliosajiliwa ni **753** (wanaume **249** na wanawake **504**).

29. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Jumla ya wagonjwa **752** waligundulika na maradhi ya kifua Kikuu (Unguja **553** na Pemba **199**). Miongoni mwa

wagonjwa hao watoto walikuwa **77**, na wagonjwa **70** walikuwa wanaishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, mgonjwa **1** kutoka Unguja aligundulika kuwa na Kifua kikuu sugu. Pia wagonjwa **50** (**44** Unguja na **6** Pemba) waligundulika na Ukoma. Wagonjwa wote hao waliogundulika wameanzishiwa matibabu ya Kifua kikuu na Ukoma.

30. **Mheshimiwa Spika,** Katika kudhibiti maradhi ya kujamiiana, jumla ya wagonjwa **2,918** (wanaume **618** na wanawake **2,300**) wamegundulika kuwa na dalili na ishara za maradhi ya kujamiiana na wote wamepatiwa matibabu. Idadi ya wagonjwa imeshuka kidogo ukilinganisha na mwaka wa 2023 ambapo jumla ya wagonjwa **2,905** (Wanaume **691** na Wanawake **2,214**) wamegundulika na kupatiwa matibabu.

31. **Mheshimiwa Spika,** Mpaka kufikia mwezi Machi 2024, jumla ya wateja **1,128** (wanaume **1,093** na wanawake **35**) wameendelea kutumia dawa kwenye kituo kinachotoa huduma ya "Methadone" katika Hospitali ya Kidongo Chekundu Unguja. Aidha kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wateja wapya **67** wamesajiliwa na kujiunga na huduma.

**HUDUMA ZA KUMALIZA MALARIA ZANZIBAR**

32. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **8,150,000,000/=** (**550,000,000/=** kutoka Serikalini na Shilingi **7,600,000,000/=** kutoka kwa

Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024, Jumla ya Shilingi **4,994,000,000/=** sawa na asilimia **61** zimeingizwa (**824,000,0000/=** kutoka Serikalini na Shilingi **4,170,000,000/=** kutoka kwa washirika wa maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali. Aidha katika kipindi cha ripoti hii, kulitokea mripuko wa ugonjwa wa malaria na Serikali ilitumia fedha zaidi ya asilimia mia moja katika ununuzi wa dawa na vipimo vya haraka vya uchunguzi wa malaria.

33. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Ugonjwa wa malaria umeongezeka kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na mwaka 2022/2023 sababu kubwa ni mabadiliko ya tabia ya nchi duniani na Zanzibar ni moja ya nchi zilizoathirika katika mabadiliko ya tabia ya nchi, jamii kusahau ugonjwa wa malaria hali ambayo imesababisha kuchelewa kufika katika vituo vya afya mapema. Kwa mwaka 2023/2024 jumla ya washukiwa **442,939** (Unguja **392,042** na Pemba **50,897**) wamechunguzwa vimelea vya malaria ambapo **19,579** (wanaume **14,569** na wanawake **5,010**) sawa na asilimia **4.42** wamegundulika kuwa na vimelea vya malaria, visa **19,074** vimegundulika Unguja. Hali hii imeonesha ongezeko kubwa ikilinganishwa na Mwaka 2022/2023 ambapo jumla ya washukiwa wa Malaria **235,862** (Unguja- **205,553** na Pemba- **30,309**) na waliogunduliwa na vimelea vya malaria ni **2,194** (Unguja **1,992** na Pemba

**202**). Katika miaka yote miwili maambukizi yameonesha kuwa makubwa sana kwa upande wa Unguja ikilinganishwa na Pemba.

34. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wagonjwa **1,593** walipata malaria kali na kulazwa katika hospitali mbalimbali za Unguja na Pemba na vifo **29** vilitokana na malaria. Aidha asilimia **82** ya maambukizo yaliyoripotiwa yanatoka Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya iliyotoa wagonjwa wengi ni Wilaya ya Mjini; asilimia **52.9** ikifuatiwa na Magharibi B asilimia **20.3**. Takwimu zimeonesha kuwa waathirika wakubwa ni wanaume wenye umri kati ya miaka 15-45 kwenye makundi ya Wanafunzi, Walinzi, Wajenzi, watembeza watalii, wenye bodaboda na baba lishe.

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kupiga dawa katika maeneo yanayotoa wagonjwa wa ndani wa malaria katika Wilaya zote **11** na kutoa elimu juu ya kinga na kumaliza ugonjwa wa malaria. Jumla ya nyumba **11,047** (Unguja **8,025** na Pemba **3,022**) kati ya nyumba **11,154** sawa na asilimia **99** ya nyumba zilipigwa dawa ya kuuwa mbu wa malaria. Aidha, Jumla ya vyandarua **93,225** (Unguja **62,265** na Pemba **30,960**) vilitolewa kwa mama wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja kupitia vituo vya afya. Jumla ya vyandarua **252,155** viligaiwa kwa jamii katika shehia **75** za Mkoa wa Mjini Magharibi kwa ajili ya kinga ya malaria. Naomba kuchukua fursa hii kuwaambia wananchi na Taasisi

husika kuwa Malaria bado ipo, hivyo jamii inapaswa kuchukua tahadhari katika maeneo yao katika kukinga Ugonjwa wa Malaria**; "Nipo tayari Kuishinda Malaria! Ziro Malaria inaanza na mimi".**

**HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO**

36. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Jumla ya shillingi **3,014,289,021/=** zimepangwa kutumika ambapo jumla ya shillingi **2,136,700,871/=** zimeingizwa sawa na asilimia **70.8** (Shilingi **250,000,000** kutoka Serikalini na Shilingi **1,886,700,871** kutoka kwa washirika wa maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza shughuli za huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto.

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika hospitali na vituo vya afya ili kufikia shabaha za malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 2030) ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia vifo chini ya **70** kwa kila kina mama **100,000**, vifo vya watoto wachanga kufikia **12** kwa kila vizazi hai **1,000** na vifo vya watoto waliochini ya miaka mitano kufikia **25** kwa kila vizazi hai **1,000** na shabaha za **Dira ya maendeleo ya Zanzibar 2050** (Zanzibar Vision 2050) ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia vifo **123** kwa kila mama **100,000** na vifo vya watoto wachanga kufikia **26** kwa kila vizazi hai **1,000** ifikapo mwaka 2030.

38. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wajawazito **41,129** walijifungulia katika vituo vya afya na hospitali Unguja na Pemba kati ya hao wajawazito **5,362** walijifungua kwa njia ya upasuaji. Aidha, wajawazito **41,289** (**41,129** walijifungua katika hospitali na vituo vya afya na **160** wamejifungulia nyumbani au wakati wakiwa wanaelekea hospitali), na wote walipatiwa huduma ndani ya masaa **48** baada ya kujifungua. **Kiambatisho nambari 2a kinafafanua zaidi.**

39. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kuekeza katika eneo la huduma za mama na mtoto na kuendelea kuimarisha utekelezaji wa afua mbali mbali zilizopelekea kupungua vifo vya mama kutoka vifo **199** kwa mwaka 2017 hadi vifo **145** kwa kila vizazi hai **100,000** kwa mwaka 2023 (DHIS-2). Aidha, kwa upande wa vifo vya watoto, vifo vya watoto chini ya miaka 5 vimepungua kutoka vifo **56** mwaka 2015 hadi vifo **47** (2022) kwa kila vizazi hai **1,000** hali hii ya kupungua kwa vifo vya mama na watoto chini ya miaka 5 inaonesha kuwa tupo kwenye muelekeo mzuri katika kufikia malengo ya "SDG" na "Zanzibar Vision 2050".

40. **Mheshimiwa Spika,** wizara kupitia mfumo wa huduma za rufaa kwa mama wajawazito na watoto wachanga (M-Mama) imeweza kusaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla

ya mama **1,556** (Unguja **1,113** na Pemba **443**) na Watoto wachanga **191** (Unguja **160** na Pemba **31**), walipatiwa huduma.

41. **Mheshimiwa Spika,** Bado kuna changamoto kwa upande wa vifo vya watoto wachanga ambapo kutoka mwaka 2015 viliripotiwa vifo **28** katika kila vizazi hai **1,000** ambapo hadi kufikia mwaka 2023 takwimu zinaonesha kuwa idadi ya vifo vya watoto wachanga bado ni **28** kwa kila vizazi hai **1,000**. Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupunguza na kuondoa kabisa vifo vya watoto wachanga ikiwemo kufanya uhakiki wa vifo ili kujua vyanzo vyake, kuhamasisha elimu ya afya kuhusu lishe, kuhudhuria mapema kliniki kwa mama wajawazito na kufuata ushauri wa wataalamu kuhusu uzazi wa mpango.

42. **Mheshimiwa Spika,** huduma za chanjo kwa makundi yote ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya watoto **55,590** (Unguja **36,234,** Pemba **19,356**) walipatiwa dozi ya tatu ya chanjo ya PENTA 3. Aidha, jumla ya wasichana **15,962** walipatiwa dozi ya pili ya chanjo ya kukinga saratani ya mlango wa kizazi (HPV2). Katika hatua nyengine jumla ya akinamama wajawazito **25,523** walipatiwa chanjo ya kinga dhidi ya pepopunda ili kumkinga mtoto mchanga mara tu baada ya kuzaliwa hadi kipindi cha mwezi mmoja. Vilevile**,** watoto **185,409** wenye umri wa miezi **6-59** wamepatiwa huduma ya ulishaji wa vitamin A na upimaji wa hali ya lishe, ambapo

ni sawa na asilimia **75** ya watoto waliotarajiwa kupatiwa huduma hio kati ya watoto **247,505. Kiambatisho nambari 2b kinatoa ufafanuzi.**

**HUDUMA ZA MARADHI YASIYOAMBUKIZA**

43. **Mheshimiwa Spika,** katika kupambana na maradhi yasiyoambukiza, wizara imeimarisha huduma za uchunguzi, matibabu na kutoa elimu ya afya kwa jamii. Jumla ya akinamama **69** waligundulika na saratani ya shingo ya kizazi kwa mwaka 2022/2023. Aidha, hadi kufikia Machi 2024 jumla ya akina mama **105** waligundulika na saratani ya shingo ya kizazi. Kwa upande wa kansa ya ya matiti mwaka 2022/2023 jumla ya akinamama **25** waliweza kugundulika na kwa mwaka 2023/2024 jumla ya wagonjwa **69** waligundulika na kansa hiyo ya matiti, takwimu zinaonyesha kuongezeka kwa maradhi hayo hivyo ni vyema kuhamasisha jamii kufanya uchunguzi mapema na kupata elimu kwani maradhi haya yanatibika endapo utagundulika kwa hatua ya awali.

44. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wagonjwa **2,209** (wanaume **725** na wanawake **1,484**) waligundulika na maradhi ya kisukari na shinikizo la damu, ambapo wagonjwa **429** (wanaume **158** na wanawake **271**) walikutwa na ugonjwa wa Kisukari na wagonjwa **1,780** (wanaume **567** na wanawake **1,213**) waligundulika na ugonjwa wa shinikizo la damu, wagonjwa wote wanaendelea kupatiwa matibabu kupitia hospitali na vituo vya afya mbali mbali Unguja na Pemba.

45. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuadhimisha wiki ya maradhi yasiyoambukiza Duniani, wizara ilifanya maadhimisho hayo kwa lengo la kutoa uelewa kuhusiana na maradhi yasioambukiza. Maadhimisho hayo yalifanyika kwa kufanya uchunguzi wa maradhi ya kisukari na shinikizo la damu ambapo watu **747** walifikiwa. Matokeo ya uchunguzi huo yameonyesha kuwa jumla ya watu **42** (**5.6%**) waligunduliwa kuwa ni washukiwa wa shinikizo la damu, na watu **5** (**0.67%**) waligunduliwa kuwa ni washukiwa wa kisukari wakiwa wote ni wanawake ambapo wagonjwa wote walipatiwa matibabu stahiki na kupewa rufaa kwa uangalizi zaidi.

**HUDUMA YA UFUATILIAJI WA MIENENDO YA MARADHI**

46. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya inaendelea kufanya ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi ambapo jumla ya visa **112,395** vya maradhi viliripotiwa kutoka vituo vya afya na hospitali ikiwemo visa vya maradhi ya kuharisha, malaria na homa ya mapafu (Nimonia). Takwimu zinaonesha kuwa ugonjwa wa kuharisha ndio unaongoza kuripotiwa kwa kuwa na visa **53,622** ukifuatiwa na ugonjwa wa homa ya mapafu yenye visa **29,765** na ugonjwa wa malaria visa **24,557**.

47. **Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji wa tetesi ya wagonjwa washukiwa wa kula vyakula vyenye sumu (Food Poisoning) yameripotiwa katika maeneo tofauti ikiwemo kuwepo kwa wagonjwa waliokuwa na dalili za kuharisha na kutapika na kuripotiwa hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja katika Wilaya

ya Mjini unaohusishwa na kula chakula chenye sumu aina ya chaza ambapo jumla ya wagonjwa **12** waliripotiwa katika tukio hilo. Ufuatiliaji umefanyika kwa kuchukua sampuli za chakula hicho ili kujuwa nini kilichosababisha kutokea kwa kadhia hiyo. Majibu kutoka kwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali yameonesha hakukuwa na sumu yoyote ya kemikali iliyokuwemo kwenye chaza hao.

48. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, kumekuwepo kwa tukio la kula kasa mwenye sumu kisiwani Pemba katika Wilaya ya Mkoani katika Kisiwa Panza ambapo jumla ya wagonjwa **257** na vifo **9** viliripotiwa kutoka katika Hospitali ya Abdullah Mzee, uchunguzi uliofanyika katika tukio hilo, matokeo yalionesha nyama ya kasa huyo alieliwa ilikuwa na sumu aina ya '*decarbamoylsaxitoxin'.* Napenda kuchukua fursa hii kuendelea kuwanasihi wananchi kuacha kuendelea kutumia kiteweo cha nyama ya kasa ili kujiepusha kupata matatizo ya kifaya na kupelekea vifo. Natoa pole kwa ndugu na jamaa wote waliopoteza ndugu na watoto wao kutokana na tukio hilo.

**HUDUMA ZA MARADHI YASIYOPEWA KIPAUMBELE**

49. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya watu **878** (Unguja **576** na Pemba **302**) walichunguzwa maradhi ya kichocho katika hospitali na vituo vya afya, kati ya hao **731** (Unguja **445** na Pemba **286**) waligundulika na maradhi hayo. Aidha, jumla ya watu **79** waliochunguzwa maradhi ya matende kati yao **33** waligundulika na vimelea vya ugonjwa huo na kupatiwa matibabu.

## HUDUMA ZA MSINGI ZA MATIBABU YA MACHO

50. **Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na mataizo ya macho kwa jamii hasa vijijini, Wizara ilifanya uchunguzi wa macho kwa watu **12,060** (wanaume **5,960** na wanawake **6,100**) katika maeneo tofauti Unguja na Pemba. Jumla ya wagonjwa **484** walipewa rufaa ya kuendelea na matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wete na Chake Chake. Aidha, jumla ya wagonjwa **345** waliweza kufanyiwa uchunguzi wa maradhi nyemelezi ya macho yanayosabishwa na matatizo ya Kisukari (Diabetic Retinopathy Screening).

## HUDUMA YA UTOAJI WA ELIMU YA AFYA NA URATIBU WA WAHUDUMU WA AFYA NGAZI YA JAMII

51. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuwafikia wananchi kuwapa elimu ya Afya, wanajamii **275,234** (Wanaume **87,632** na Wanawake **187,602**) wamefikiwa na kupewa elimu ya afya ya kujikinga na magonjwa ya Malaria, Kipindupindu, athari za kiafya zinazotokana na Udhalilishaji na Unyanyasaji wa watoto, Usafi wa Mazingira, Uchangiaji Damu, Matumizi ya dawa za kutibu maji, Maradhi yasiyoambukiza, Uzazi wa mpango, Makuzi na malezi, kinga dhidi ya maradhi ya mripuko kwa jamii, Saratani na Lishe.

52. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha elimu ya afya inawafikia walengwa wengi zaidi katika jamii, Wizara imeweza kutoa elimu ya afya katika maskuli ambapo jumla ya Skuli

**336** na wanafunzi **54,357** (Wanaume **23,241** na Wanawake **31,116**) wameweza kufikiwa Unguja na Pemba. Mada mbali mbali ziliwasilishwa zikiwemo, umuhimu wa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana, Usafi wa Kinywa na meno, Kinga dhidi ya Malaria, Utunzaji wa mazingira, Ugonjwa wa Kipindupindu, Usafi na matumizi sahihi ya vyoo na Lishe bora. Aidha elimu ya afya ilitolewa kuhusiana na maradhi yasiyoambukiza katika Skuli za Sekondari na Vyuo ambapo jumla ya wanafunzi **2,637** walifikiwa na kupatiwa elimu kuhusiana na maradhi yasiyoambukiza na vichocheo vyake.

53. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuelimisha jamii kupitia vipindi vya Redio **234** kupitia Redio Nuru FM, Adhana FM, Zenji FM, Kati FM, Mtegani FM, Tumbatu FM, ZBC, Micheweni, Mkoani na kwa upande wa vipindi vya TV jumla ya vipindi **62** vimerushwa kupitia ZBC TV na ZCTV. Vilevile, vipindi **299** viliandaliwa kuhusu afya ya akili ambavyo vililenga madrasa, vikundi maalum kwenye jamii, wanafunzi wa sekondari na vyuo, ambapo jumla ya washiriki **7,525** walifaidika na elimu iliyotolewa. Vilevile elimu kama hizi ziliweza kutolewa kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii ikiwemo Afya-Online-TV, Twiter, Facebook, Whatsapp, na Magazeti mbalimbali nchini. Vilevile wizara imeweza kuanzisha STUDIO maalum ya kurikodi na kuandaa vipindi mbalimbali vya elimu ya afya zaidi ya vipindi **210** vimeandaliwa na kurushwa kupitia mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa Online-TV.

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara baada ya kuona kumekua na ongezeko la magonjwa ya miripuko duniani ikiwemo nchi yetu, iliamua kuanzisha kituo maalumu cha kuripoti na kupokea habari za magonjwa ya miripuko na dharura yaani **AFYA CALL CENTER** chenye lengo la kuisaidia jamii kupata sehemu ya kuripoti pale yanapotokea magonjwa ya miripuko na dharura na kuchukua hatua stahiki. Kuanzia mwezi machi 2024 kituo kimeanza kazi kwa masaa **12** kwa kutumia namba ya dharura (**190**) ili kuripoti na kuuliza masuala mbalimbali ya kiafya, zaidi ya wananchi **1,200** wamepiga simu kituoni hapo kwa ajili ya kupata huduma hizo.

55. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Pili Rais na washirika wa maendeleo inaendelea kutekeleza mpango wa miaka minne (**4**) wa urasimishaji wa wahudumu wa afya wakujitolea kuwa kada rasmi ya afya ngazi ya jamii. Mpango huu ulizinduliwa rasmi na **Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** siku ya tarehe 16 Disemba 2023.

56. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la kuwa na wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni kuimarisha huduma ya afya ya msingi jumuishi ili kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi kwa urahisi baadhi ya huduma hizo ni mama na mtoto, lishe, uhamsishaji wa chanjo, upimaji wa malaria, upimaji wa shinikizo la damu na kisukari Wizara inaendelea na hatua za kuwajengea uwezo na kuongeza idadi ya wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii kutoka **2300** hadi kufikia **3,000** ifikapo 2026.

**HUDUMA ZA AFYA YA MAZINGIRA**

57. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wananchi wanatumia maji safi na salama, jumla ya sampuli **61** za maji zilichukuliwa kutoka visima vya watu binafsi kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara. Matokeo ya uchunguzi huo yameonesha kuwa jumla ya sampuli **34** zimebainika kuwa na vimelea vinavyosababisha maradhi ya kuharisha na sampuli **27** hazikuwa na vimelea. Hatua za kuwapatia elimu wamiliki wa visima hivyo juu ya utaratibu wa kutibu maji zilichukuliwa pamoja na kuwapatia vidonge vya kutibu maji.

58. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, jumla ya vidonge **32,780** vimegawiwa kwa ajili ya kutibu maji kwa wenye visima na matangi ya kuhifadhia maji ili kupunguza athari zitokanazo na mvua na kupelekea magonjwa ya kuharisha ikiwemo Kipindupindu. Sambamba na hilo, uhamasishaji jamii umefanyika katika ujenzi wa vyoo katika nyumba **108** ambazo zilibainika kutotumia vyoo vilivyo bora katika tathmini iliyofanyika mwaka wa fedha 2022/2023. Jumla ya vyoo vya aina ya 'SATO PAN' **4,874** (Unguja **3,463** na Pemba **1,411**) vimetolewa ili kupunguza idadi ya nyumba ambazo hazina huduma ya vyoo na kuweza kuepukana na magonjwa ya miripuko ikiwemo Kipindupindu.

59. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya maeneo **539** ya biashara ikiwemo mikahawa, vioski, hoteli, bekari na maeneo ya skuli yamefanyiwa ukaguzi kuangalia utekelezaji wa kanuni na

miongozo ya afya katika maeneo ya kutolea huduma ya chakula. Matokeo ya ukaguzi huo umebaini kuwa maeneo yote yaliyokaguliwa yameonekena kuwa na changamoto za kutofuata kanuni na miongozo ya afya katika maeneo ya kutolea huduma.

60. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa kasoro zilizojitokeza ni pamoja na watoa huduma kutokuwa na utamaduni wa kupima afya zao, kutovaa sare, uuzaji wa vyakula vilivyokaa muda mrefu, ukosefu wa maji safi na salama, kutokuwepo ndoo maalumu za kuhifadhi taka na kukosekana huduma za vyoo katika maeneo yao hali ambayo ni hatari kwa afya ya jamii. Hatua zilichukuliwa ni pamoja na kuviteketeza vyakula vilivyokaa muda mrefu (viporo), kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria kulingana na makosa husika.

**HUDUMA ZA AFYA MIPAKANI (BANDARINI NA VIWANJA VYA NDEGE)**

61. **Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa vyombo vya usafiri vilivyoingia nchini pamoja na abiria ulifanyika, ambapo jumla ya vyombo **31,766** vilikaguliwa, kati ya hivyo **25,486** ni vya anga na **6,280** vya usafiri wa baharini. Vyombo **5** vya baharini vilibainika kuwa na mapungufu ya kiafya na hatua zilichukuliwa kwa kutoa elimu ya afya na kupiga dawa.

62. **Mheshimiwa Spika,** Aidha ukaguzi wa abiria kupitia vyombo vya usafiri ulifanyika ambapo jumla ya abiria walioingia nchini na kukaguliwa ni **1,507,533** kati ya hao **1,111,976**

walikuwa wenyeji na **395,557** walikuwa ni wageni, ambapo zaidi ya wasafiri **238** walibainika kuwa na joto kubwa la mwili zaidi ya nyuzi joto **38** walipofanyiwa uchunguzi wa awali. Baada ya kufanyiwa upimaji joto wa marejeo **102** waligunduliwa kuwa na Malaria ambapo walipatiwa huduma ya kwanza na wameripotiwa kama miongozo inavyoelekeza, na waliobaki walibainika kuwa na joto la kawaida kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ya joto.

63. **Mheshimiwa Spika,** Chanjo kwa wasafiri zimeendelea kutolewa ambapo jumla ya dozi **12,810** zimetolewa, kati ya hizo, dozi **4,145** ni za UVIKO-19, dozi **7,297** ni za homa ya manjano, dozi **33** za homa ya uti wa mgongo na dozi **1,335** za homa ya Ini B. Aidha ukaguzi wa maiti na wagonjwa ulifanyika ambapo jumla ya wagonjwa **694** na maiti **140** walipitishwa na kukaguliwa kupitia bandarini na viwanja vya ndege. Hakukua maiti aliebainika na dalili za magonjwa ya kuambukiza.

**HUDUMA YA AFYA YA WAFANYAKAZI**

64. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wafanyakazi kwenye taasisi za umma na binafsi wanatoa huduma wakiwa na afya bora na salama wizara kupitia kitengo cha huduma ya afya kwa wafanyakazi kimefanya uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi **27,682**, kati yao wafanyakazi **3,462** walibainika kuwa na matatizo mbali mbali ya kiafya yakiwemo maradhi ya maambukizi ya mkojo, shinikizo la damu, uoni hafifu, Pumu, Homa ya Ini aina "B", Kisukari, Maradhi ya Ngozi,

Homa ya Ini “C”, HIV na Kaswende. Wagonjwa wote waliobainika kuwa na matatizo walipatiwa ushauri na rufaa kwenda kupata huduma stahiki.

65. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) imeweza kufanya uchunguzi wa Afya kwa wafanyakazi ili waweze kulipwa stahiki zao kwa waliopata ajali kazini. Jumla ya wafanyakazi **31** wamejaziwa fomu za fidia ili waweze kupata stahiki baada ya kupata ajali wakiwa kazini.

**HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI YA AKILI**

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeimarisha huduma za afya ya akili kwa kuhakikisha kwamba vituo **34** vya afya ya msingi (Health Centers) vinatoa huduma za afya ya akili Unguja na Pemba. Aidha, kwa kipindi cha Julai 2023 hadi machi 2024, jumla ya wagonjwa wa afya ya akili **474** (wanaume **316** na wanawake **158**) wamepatiwa matibabu ya nje (OPD) kwenye kliniki ya afya ya akili Kidongo Chekundu. Vilevile Jumla ya wagonjwa **245** (Wanaume **181** na Wanawake **94**) wamelazwa katika hospitali ya wagonjwa wa akili Kidongo Chekundu kwa matatizo mbali mbali ya afya ya akili ikiwemo; mpasuko wa mawazo(schzophenia), Watumiaji wa madawa sugu (drug induced sychosic) na Sonona (depression).

67. **Mheshimiwa Spika,** Maadhimisho ya Siku ya Afya ya Akili Duniani yaliadhimishwa kwa shughuli mbali mbali zikiwemo utoaji wa elimu ya afya ya akili kupitia mashuleni, hospitali

ya wagonjwa wa akili Kidongo Chekundu na familia za wazazi na ndugu wenye matatizo ya afya ya akili, ambapo jumla ya wahusika **300** katika jamii walinufaika na elimu hiyo ili kukabiliana na ugonjwa wa afya ya akili. Aidha jumla ya wafanyakazi **203** wa kada za afya na ualimu waliweza kupatiwa mafunzo hayo kuhusu afya ya akili.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya watu **20,100** wamepatiwa elimu ya afya ya akili Unguja na Pemba kupitia mradi wa "Pamoja Afya Bora", lengo ni kufikia watu **90,000** ifikapo mwezi Oktoba, 2025. Lengo la mradi huu ni kuzidisha uelewa wa jamii juu ya afya ya akili na kupunguza unyanyapaa kwa watu wenye matatizo ya afya ya akili Zanzibar.

## UTEKELEZAJI WA BODI NA MABARAZA YA TAALUMA ZA AFYA

### *BARAZA LA TAALUMA ZA AFYA YA JAMII NA MAZINGIRA*

69. **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024 Baraza limeweza kusimamia taaluma za kada ya Afya ya Jamii na Mazingira kwa kutoa usajili na leseni za kazi kwa Maofisa wa Afya ya Jamii na Mazingira. Jumla ya leseni **172** (**114** kuhuwisha na **58** leseni mpya) za Maafisa Afya zimeweza kusajiliwa kwa ngazi mbali mbali za shahada ya uzamili, shahada ya kwanza na stashahada.

**PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA (PH0102)**

70. **Mheshimiwa Spika,** jukumu la Programu hii ni kuhakikisha jamii inapata huduma bora za tiba katika hospitali za wilaya na mikoa. Utekelezaji wa shughuli za Programu hii umegawika katika program mbili ndogo: Programu ya Huduma za Matibabu na Programu ya Huduma za Uchunguzi. Kwa mwaka wa fedha 2023/ 2024, Programu ya Tiba ilipangiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu katika hospitali za wilaya na mkoa;
ii. Kutekeleza mfumo wa rufaa kwa wagonjwa katika ngazi zote za utoaji wa huduma;
iii. Kuimarisha kambi za matibabu na mashirikiano ya huduma za afya kimataifa;
iv. Kuongeza ukusanyaji wa damu ili kukidhi mahitaji yaliyopo;
v. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa tiba na vitendanishi (reagents);
vi. Kuimarisha huduma za uchunguzi (maabara na rediolojia);
vii. Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoajiwa huduma za Afya;
viii. Kuimarisha usimamizi katika uhifadhi na utumiaji wa dawa na vifaa vya utibabu katika hospitali na vituo vya afya;
ix. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wahanga wa udhalilishaji; na
x. Kuimarisha uratibu wa huduma za uuguzi na ukunga.

71. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu (PH0102) limepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **90,490,626,000/=** ambapo Shilingi **86,911,126,000/=** kwa ajili ya huduma za matibabu na Shilingi **3,579,500,000/=** kwa ajili ya huduma za uchunguzi. Hadi kufikia Machi 2024 Programu hii iliingiziwa kiasi cha Shilingi **45,720,454,068/=** sawa na asilimia **46.9**, kati ya hizo Shilingi **40,812,065,304/=** zilizoingizwa kwa ajili ya huduma za matibabu na Shilingi **4,908,388,764/=** kwa ajili ya huduma za uchunguzi.

**PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA MATIBABU**

72. **Mheshimiwa Spika,** Huduma za matibabu ya Wagonjwa wa nje (Outpatient) na wagonjwa wa kulazwa (Inpatient) zinaendelea kutolewa katika hospitali za Mkoa, Wilaya na hospitali za binafsi. Jumla ya mahudhurio ya wagonjwa wa nje ni **406,598** (Wanaume **160,441 n**a Wanawake **246,157**)**,** kwa wagonjwa waliolazwa kwa matatizo mbali mbali ya kiafya ni **22,225** (Wanaume **10,039 n**a Wanawake **12,186).** Aidha wagonjwa **632** (Wanaume **358 n**a Wanawake **274**) wamefariki dunia sababu kuu ya vifo hivyo ni pamoja na Kiharusi, ubongo kukosa hewa wakati wa kuzaliwa watoto, upungufu mkubwa wa damu, homa kali ya mapafu kwa watoto, moyo kushindwa kufanya kazi na figo kushindwa kufanya kazi. Jumla ya ajali **409** zimeripotiwa kati ya hizo ajali **301** ni ajali za barabarani na **108** ni ajali nyenginezo.  Vile vile jumla wagonjwa **13** wanaendelea

kupata huduma ya kusafisha damu "dialiysis" katika Hospitali ya Abdulla Mzee. Aidha mahudhurio ya wagonjwa **82,284** (Wanaume **35,093** na Wanawake **47,191**) **wameripotiwa** katika klinik za maradhi maalumu kwa Unguja na Pemba kliniki hizo zinajumuisha magonjwa ya Kisukari, Shinikizo la damu, moyo na mengineyo. **Viambatisho nambari 3a na 3b vinafafanua zaidi.**

**HUDUMA ZA UCHUNGUZI**

73. **Mheshimiwa Spika,** Huduma za uchunguzi ni huduma zinazojumuisha uchunguzi wa maradhi kwa kutumia sampuli za aina mbalimbali zinazotokana na binaadamu. Uchunguzi huu hufanyika katika na uchunguzi wa njia picha (Radiology and Imaging Services) zikiwemo X-ray, Ultrasound, CT scan na MRI. Huduma hizi hutolewa katika hospitali za serikali na zile za binafsi. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Wizara imefanikiwa kupima wagonjwa vipimo **636,536** (Maabara **556,389,** Njia ya picha **80,147**), kipimo kinachoongoza kwenye maabara ni vipimo vya kemia ambapo kipimo kwa njia ya picha ni Ultra-Sound ikifuatiwa na X Ray. Vipimo hivyo vimefanyika katika Hospitali zote za Unguja na Pemba. **Kiambatisho nambari 3c kinafafanua**.

**HUDUMA ZA USHIRIKIANO WA AFYA KIMATAIFA**

74. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya na Washirika wa Maendeleo mbali mbali wa ndani na nje ya nchi walifanya kambi za matibabu ya magonjwa mbali mbali. Kwa kipindi

cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya kambi **23** zilifanyika Unguja na Pemba katika hospitali za wilaya, mkoa na rufaa ambapo wanachi **16,328** walipatiwa huduma za uchunguzi na matibabu kwa maradhi mbali mbali ikiwemo mifupa, matibabu ya macho, upasuaji wa jumla, maradhi ya kina mama, mfumo wa mkojo, uchunguzi wa saratani ya matiti na shingo ya kizazi na ngozi.

75. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya Wagonjwa **375** wamepatiwa rufaa kwenda Tanzania Bara kwa matibabu zaidi, katika hospitali ya Taifa Muhimbili, MOI, JKCI, Ocean Road na KCMC ambapo kiasi cha Shilingi **2,400,000,000/=** zilitumika. Aidha jumla ya wagonjwa **113** (**66** wapya na **67** wamarudio) walipatiwa rufaa kwenda hospitali ya MIOT- India kwa ajili ya matibabu ya ziada ikiwemo magonjwa ya mifupa, saratani, moyo na maradhi ya macho jumla ya Shilingi **4,000,000,000/=** zilitumika. **Kiambatisho nambari 3d kinafafanua zaidi**.

**HUDUMA ZA DAMU SALAMA**

76. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya uniti za damu **11,811** kwa wachangiaji wa hiari. Hii ni sawa na asilimia **79** ya uniti za damu ambapo lengo lilopangwa ni kukusanya uniti **15,000** za damu. Jumla ya uniti **12,954** sawa na asilimia **33** kati ya maombi ya uniti **38,595** ya damu zilisambazwa katika hospitali za umma na hospitali binafsi

kwa matumizi mbali mbali. Ukusanyaji huu ulifanikishwa kupitia uhamasishaji kwenye jamii kwa kurusha vipindi kupitia Redio na TV pamoja na mabonanza ya uchangiaji damu yaliyofanyika katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba.

## HUDUMA ZA MKONO KWA MKONO (ONE STOP CENTRE)

77. **Mheshimiwa spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya matukio ya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto **2,957** yaliyoripotiwa ikiwemo; Udhalilishaji wa Kimwili matukio **36**, udhalilishaji wa kingono **537**, Udhalilishaji wa kihisia **388**, Kulawitiwa **523**, Jaribio la kubakwa na Kulawitiwa **92**, Kukashifiwa **1,225** na Ujauzito **156**. Idadi hiyo inaonekana kupanda ikilingwanishwa na mwaka jana ambapo matukio ya udhalilishaji **1,217** yaliripotiwa. Wahanga wa matukio yote hayo walipatiwa huduma za afya stahiki. **Kiambatatisho nambari 3e kinafafanua.**

## HUDUMA ZA BODI NA MABARAZA YA TAALUMA ZA AFYA

### *BODI YA USHAURI YA HOSPITALI BINAFSI*

78. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi iliyoanzishwa kwa Sheria Na. **4** ya Mwaka 1994 pamoja na mambo mengine ina jukumu la kusajili na kusimamia vituo vya afya binafsi. Hadi kufikia machi 2024, Bodi imefanikiwa

kusajili jumla ya vituo **284** (**176** vinafanya kazi, **98** vimefungwa moja kwa moja na **10** vimefungwa kwa muda ili kupewa muda wa kujirekebisha). Vituo vinavyofanya kazi ni; Hospitali **5,** Vituo vya Afya **4**, Zahanati **120,** Kliniki **11,** Polyclinics **10**, Maabara Binafsi **3,** Kliniki za huduma ya kwanza **22** na kituo cha uchunguzi kimoja.

**79. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya maombi **20** ya vituo binafsi yaliwasilishwa; maombi **19** yalikuwa maombi ya vituo vipya, ombi **1** lilikuwa la kituo kinachoomba kupandishwa daraja. Aidha, vituo **11** vilikidhi vigezo vya kusajiliwa, vituo **4** vilikuwa na mapungufu mbalimbali yaliyohitaji kuboreshwa na vituo **3** havikukidhi vigezo.

**80. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu na kuhakikisha huduma za afya katika hospitali binafsi zinaboreshwa, Bodi ya Ushauri Hospitali binafsi imefanya ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma za afya binafsi katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Jumla ya vituo **50** vimekaguliwa ambapo jumla ya vituo **5** vilisitishwa kutoa huduma kutokana na mapungufu mbalimbali ikiwemo uhaba mkubwa wa wafanyakazi, miundombinu chakavu, kutokuwa na vifaa tiba na kutozingatia miongozo ya kukinga na kuzuia maambukizi.

### *BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA ZA TIBA*

81. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la wataalamu wa maabara za Tiba hadi sasa limeshasajili jumla ya wataalamu wa Maabara **602** (Unguja **447** na Pemba **155**) Aidha, jumla ya wataalamu **225** waliwasilisha maombi yao ya usajili na kupatiwa usajili kama sheria inavyoeleza. Sambamba na hilo, Baraza limefanikiwa kufanya ukaguzi wa vituo **114** (Unguja-**64** na Pemba-**50**) kati ya vituo **363** vya umma na binafsi vinavyotoa huduma za maabara. Lengo la ukaguzi huu ni kuweza kutambua watalamu wanaofanya kazi kuwa wamesajiliwa kisheria. Matokeo yameonyesha kuwa kati ya watalamu **448** (Unguja-**303** na Pemba-**145**) wataalamu **329** wamesajiliwa na watalaamu **119** (Unguja-**204** na Pemba **125**) hawakusajiliwa hivyo walikamilisha taratibu za usajili baada ya ukaguzi huo.

### *BARAZA LA TIBA ASILI NA TIBA MBADALA*

82. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala limeweza kufanya usajili wa maeneo **1,027** zikiwemo; Klinik za Tiba Asili (**59**), Kliniki za Tiba Mbadala **6**, Maduka ya Dawa Asili **259**, Waganga (**564**) Wasaidizi waganga (**191**) na Ghala **(3)**. Aidha, Baraza limefanya ukaguzi katika maeneo **282** Unguja na Pemba. Ukaguzi huu ulijumuisha vituo vya Tiba Asili (**64)**, Kliniki (**20**), Maduka ya Dawa Asili (**142**) na Waganga wa Tiba Asili (**56)**. Aidha ukaguzi uliendelea katika maeneo mengine yakiwemo Masoko, Majengo ya Ibada,

sehemu za maonesho na maeneo yenye mikusanyiko ya watu, jumla ya maeneo (**15)** yalifungiwa kwa sababu ya kukosa vigezo vikiwemo kutosajiliwa au kutohuisha vibali.

83. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanya uhuishaji vibali (renewal) vya Kliniki za Tiba Asili **5**, Maduka ya Dawa Asili **13**, Waganga **12** na Wasaidizi waganga **2,** Aidha Baraza limefanikiwa kutoa vibali **6** vya kuingiza dawa asili nchini "Import Permits", ambapo dawa hizo zimetoka nchini India na Uturuki. Katika hatua nyengine vibali **20** vya kusafirisha dawa za asili nje ya nchi "Export Permits" vimetolewa baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kiusalama na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Dawa hizo zilisafirishwa kwenda nchini Ujerumani, Uengereza, Marekani, Canada na Oman. Wizara inatoa wito kwa wananchi wasitumie dawa za asili kiholela bali wahakikishe wanafuata ushauri wa wataalamu na kutumia dawa hizo kutoka katika maeneo yaliyosajiliwa.

***BARAZA LA MADAKTARI***

84. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Madaktari lina jukumu la kusimamia na kudhibiti taaluma ya udaktari pamoja na kuhakikisha madaktari wanatoa huduma kwa kufuata maadili ya kazi hiyo. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Baraza limefanikiwa kusajili na kutoa leseni kwa madaktari wapya **380** (Wazalendo **371** na Wageni **9**) na jumla ya madaktari **1,418** (Wazalendo **1,395** na Wageni **23**) walihuisha leseni zao.

***BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA***

85. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lina jukumu la kusimamia na kudhibiti Taaluma ya Uuguzi na Ukunga pamoja na kuhakikisha Wauguzi na Wakunga wanatoa huduma kwa kufuata Maadili na Miongozo ya kazi hiyo. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Baraza la Wauguzi na Wakunga limefanikiwa kusajili na kuwapa leseni Wauguzi wapya **270** sawa na asilimia (**77**) kati ya Wauguzi **350** waliotarajiwa kusajiliwa. Aidha, Wauguzi **411** wamehuisha leseni zao sawa na asilimia (**40**) kati ya Wauguzi **1,035**, vile vile kwa mwaka huu Baraza halikupokea malalamiko yanayohusu hali ya upatikanaji wa huduma usioridhisha kwa Wananchi. Hadi sasa Baraza limesajili jumla ya wauguzi **3,106** (**2,248** walioajiriwa na Serikali na **858** wa sekta binafsi).

**HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA**

86. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha huduma za Uuguzi na Ukunga zinatolewa kwa ubora katika ngazi zote. Serikali ya awamu ya **nane (8)** imeanzisha Idara maalumu ya Uuguzi na Ukunga kwa lengo la kusimamia ubora katika utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga katika ngazi zote zinazotolewa huduma za afya.  Sambamba na hilo, Wizara ya Afya, katika kuhakikisha miongozo ya kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga inatekelezwa; imeandaa miongozo mbalimbali ikiwemo; muongozo wa mafunzo ya Uuguzi na Ukunga, muongozo wa muundo wa uongozi wa Idara ya Uuguzi na Ukunga na muongozo wa watoa huduma za Uuguzi na Ukunga.

87. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilifanikiwa kufanya uhakiki wa kukusanya taarifa zote za wauguzi walioajiriwa na Wizara ya Afya kwa lengo la kujua idadi halisi ya wauguzi waliopo kwenye hospitali na vituo vya afya vya serikali. Jumla ya wauguzi **1,799** (Unguja **1,301** na Pemba **498**) wameajiriwa. Uhakiki huo unaonyesha kuwa bado kuna upungufu mkubwa wa wauguzi hali inayopelekea kutokufikia lengo la utoaji wa huduma bora. Aidha, uhakiki huo umebaini kuwa idadi kubwa ya wauguzi wana elimu ya ngazi ya Stashahada.

88. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuwajengea uwezo viongozi wa Uuguzi na Ukunga, Wizara iliweza kuendesha mafunzo ya Uongozi kwa viongozi wenye dhamana kwenye hospitali na vituo vya afya. Jumla ya viongozi **20** wa Uuguzi na Ukunga walipatiwa mafunzo hayo. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajenga uwezo katika kusimamia watendaji wanaowaongoza na kuhamasisha kwa vitendo timu zao kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuzingatia mifumo ya kisasa na ya kimataifa ili waweze kutoa huduma bora zenye kujali utu kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na yale ya Uuguzi na Ukunga.

## HUDUMA YA UPATIKANAJI, UHIFADHI, USAMBAZAJI WA DAWA NA VIFAA TIBA

### *OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI*

89. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali, inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Dawa (National Medicine Policy 2021) kwa kuimarisha huduma za upatikanaji wa dawa muhimu, vifaa tiba pamoja na kusimamia matumizi sahihi ya dawa. Sambamba na hilo, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbali mbali walifanya makisio ya dawa kwa kutumia njia mpya ya ukusanyaji wa taarifa za dawa na vifaa tiba kuanzia ngazi za vituo vya afya na Hospitali zote kwa lengo la kuboresha taarifa sahihi na kuwawezesha kufanya maoteo yao wenyewe ili kuweza kwenda sambamba na mabadiliko yanayoendelea na kuboresha huduma bora za afya kwa jamii.

90. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeandaa miongozo mbali mbali ikiwemo mwongozo wa matibabu nchini (Standard Treatment Guidelines 2024) na Orodha ya Dawa Muhimu (Essential Medicines List 2024), muongozo huu uliangalia mabadiliko yote yanayoendelea ya afya nchini na wataalamu mbali mbali kutoka sekta ya afya na washirika wa maendeleo walishiriki kuandaa mwongozo huo, kwa sasa muongozo huo umeshaanza kutumika Zanzibar. Aidha, ofisi iliandaa miongozo ya kuchakata taarifa za dawa za kufanya maamuzi sahihi ya taarifa za ugavi wa dawa na vifaa tiba (Supply Chain) katika ngazi zote za utoaji wa huduma.

**91. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024**,** Wizara imepangiwa jumla ya Shilingi **20,475,000,000/=** kwa ununuzi wa dawa na vifaa tiba ambapo Shilingi **20,098,370,995/=** sawa na asilimia **98** kati ya hizo Shilingi **8,786,271,018/-** zilitumika kwa ununuzi wa dawa kwa vituo vya Afya na Shilingi **6,753,728,982/=** zilitumika kwa malipo ya watoa huduma binafsi katika Hospitali za Umma "Outsourcing" na Shilingi **4,558,370,995/=** zilitumika kwa ulipaji wa madeni ya zamani ya dawa na vifaa tiba. Aidha, fedha zilizoingizwa zimeongezeka kwa asilimia **67.6** ukilinganisha na mwaka 2022/2023 ambazo zilikuwa ni Shilingi **6,850,000,000/=**, ongezeko hili limepelekea kuengezeka kwa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya.

### *WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA*

**92. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuifanya Bohari Kuu ya Dawa kuwa Wakala ambapo majukumu yake ni pamoja na kununua, kutengeneza, kuuza, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa vya utibabu na vitendanishi.

**93. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Bohari Kuu ya Dawa Maruhubi imepokea dawa muhimu, vitendanishi (reagents) na vifaa vya utibabu vyenye thamani ya Shilingi **23,647,577,872.52/=** ambapo jumla ya Shilingi **15,293,151,110.56/=** kupitia fedha za SMZ na Shilingi **8,354,426,762/=** kupitia fedha za Washirika wa Maendeleo.

94. **Mheshimiwa Spika**; Kwa upande wa Bohari ya Maruhubi jumla ya maeneo **137** yanayotoa huduma mbali mbali yalisambaziwa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi **13,016,440,693/=.** Vilevile, Bohari ya Vitongoji maeneo **82** yanayotoa huduma mbali mbali yalisambaziwa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi **985,211,956.16/=.** Aidha, Bohari Kuu ya Dawa Vitongoji imepokea dawa muhimu zenye thamani ya Shilingi **1,452,455,045.55/=** kupitia fedha za SMZ. Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa inaendelea na utaratibu wa usambazaji wa dawa na vifaa tiba kila mwezi kwa vituo vyote vya afya na hospitali ili kuimarisha upatikanaji wa dawa kuondosha usumbufu kwa wananchi.

## PROGARAMU NDOGO YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI (SH030202)

### *HUDUMA ZA WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI*

95. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ilikagua jumla ya maeneo ya biashara za chakula, Dawa, vipodozi na vifaa tiba **2,762** (Unguja **1,683** na Pemba **1,079**)**.** Aidha, jumla ya maeneo **525** (Unguja **404** na Pemba **121**) yamesajiliwa. Vilevile, jumla ya maombi ya usajili wa bidhaa **59** yalipokelewa kati ya hayo maombi **42** yamesajiliwa baada ya kuonekana yamekidhi viwango vya usajili.

96. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya sampuli **1,200** kati ya sampuli **2,960** sawa na asilimia **41** zikiwemo Chakula **1,064**, Dawa **44**, Vipodozi **86** na Vifaa Tiba **6** zilifanyiwa uchunguzi ambapo sampuli **41** (chakula **36**, dawa **3** na vipodozi **2**) hazikufikia viwango vilivyowekwa na kugundulika hazifai kwa matumizi ya binaadamu. Aidha, Wakala wa chakula, dawa na vipodozi imekuwa mwanachama kamili wa Programu ya kimataifa ya ufuatiliaji usalama wa dawa wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO).

### *HUDUMA ZA WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI*

97. **Mheshimiwa Spika,** Katika kufanya uchunguzi wa sampuli, Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepokea sampuli **243** za kesi za jinai zikiwemo za

dawa za kulevya aina ya unga, bangi, mkojo na shisha kwa ajili ya kuzifanyia uchunguzi na kutoa ripoti kwa wakati. Aidha sampuli **296** za bidhaa za chakula na dawa zikiwemo asali, maji ya chupa, maji ya kisima na tomato sauce kwa ajili ya kufanya uchunguzi ili kufahamu kama zinafaa kwa matumizi ya binaadamu.

98. **Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyengine wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imefanya udhibiti wa kemikali ambapo vibali **1,764** vya uingizaji, usambazaji na utoaji wa kemikali na bidhaa zinazotokana na kemikali vimetolewa. Kati ya vibali hivyo, vibali **1,715** ni vya uingizaji wa kemikali, **40** vya utoaji wa kemikali na **9** vya usafirishaji wa kemikali. Vile vile Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imefanikiwa kufanya usajili wa maeneo mapya **62** na maeneo **77** yamehuisha usajili. Jumla ya maeneo **208** ya kuhifadhi kemikali yamefanyiwa ukaguzi.

99. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imefanya uchunguzi wa sampuli **812** kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Mach 2024. Katika uchunguzi wa sampuli hizo sampuli **336** ni za makosa ya jinai, sampuli **130** ni za Kemikali na bidhaa zitokanazo na kemikali, na sampuli **346** ni za chakula na dawa. Aidha katika kufanya uchunguzi wa sampuli hizo sampuli **676** zimekidhi viwango na jumla ya sampuli **136** hazikukidhi viwango. Hatua

zilizochukuliwa kwa sampuli ambazo hazikukidhi viwango ni kuwaelimisha wateja njia gani watumie ili kuzifanya bidhaa zao zifikie viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

**100. Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia na kudhibiti kemikali na bidhaa za kemikali Zanzibar, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imedhibiti Kemikali na bidhaa za kemikali kwa kufanya kaguzi katika maeneo ya Bandari na Maghala ya kuhifadhia kemikali. Aidha, jumla ya kaguzi **562** zimefanyika na kutoa jumla ya vibali **2,642** vya umiliki wa kemikali pamoja na kusajili wadau wapya **71** na wadau **87** walipata usajili wa uhuwishaji (renewal). Aidha naipongeza taasisi kwa juhudi kubwa wanazozichukua na kuendelea kufanikisha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na pia nawaomba wananchi waendelee kuhamasika kuitumia na kujenga imani na matokeo ya sampuli yanatolewa na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA (PH0103)

**101. Mheshimiwa Spika,** Programme ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya kwa mwaka fedha 2023/2024 ilipangiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kupeleka masomoni Madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

ii. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali zikiwemo tafiti za mimea inayotumika kwa Tiba asili;

iii. Kufanya vikao vya pamoja na washirika mbali mbali wa masuala ya Afya ili kutatua changamoto kwa nguvu ya pamoja;

iv. Kufanya ufuatiliaji wa sera na miongozo ya utoaji huduma za afya;

v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za utoaji wa huduma; na

vi. Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu za afya

## PROGRAMU NDOGO YA UTAWALA NA UENDESHAJI (SH010301)

**102. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, programu hii ilitengewa kutumia kiasi cha Shilingi **9,878,103,460/=** hadi kufikia Machi 2024 programu iliingiziwa na kutumia jumla ya Shilingi **6,330,635,734/=** sawa na asilimia **64.**

## NGUVU KAZI YA SEKTA YA AFYA

**103. Mheshimiwa Spika**, Mpaka kufikia Machi 2024 Wizara ina jumla wafanyakazi **7,519** (Unguja **5,657** na Pemba **1,862**). Aidha wizara imeajiri jumla ya wafanyakazi **95** wa fani tofauti ambao tayari wameshasambazwa katika hospitali na vituo vya Afya. **Kiambatisho nambari 4a kinafafanua zaidi.**

**104. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha wafanyakazi wanaoajiriwa wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni za utumishi, wizara imewapatia mafunzo elekezi (Induction Course) jumla ya wafanyakazi **207.** Vilevile wafanyakazi **596** wanatarajiwa kufanyiwa mafunzo elekezi kwa kipindi cha robo ya nne. Aidha, wafanyakazi **88** wamestaafu kwa mujibu wa kanuni na sheria za Utumishi wa umma, wafanyakazi **9** wamechukua likizo bila ya malipo na wafanyakazi **6** wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu peponi, Amin.

105. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilitenga jumla ya Shilingi **2,000,000,000/=** kwa ajili ya kusomesha na kuendeleza wafanyakazi. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya Shilingi **1,321,961,600/=** zimetumika sawa na asilimia **66** ambapo watumishi **252** (**229** kada za afya na **29** kada nyenginezo) wamepewa ruhusa ya kwenda masomoni na kufanya idadi ya watumishi waliopo masomoni kufikia **726** (**672** kada za afya na **54** kada nyenginezo) katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi. **Kiambatisho nambari 4b kinafafanua zaidi.**

**USIMAMIZI WA SHERIA**

106. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2023/2024, Wizara imeandaa sheria mbili **(2)** na kupitishwa na Baraza lako tukufu. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mfuko wa huduma za Afya na Sheria ya Wakala wa Bohari kuu ya Dawa. Aidha kanuni za ujumla za mfuko wa huduma za afya na kanuni za ujumla za udhibiti wa Hospitali Binafsi zimeandaliwa.

107. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeingia makualiano na Mashirika ya ndani na nje ya nchi kupitia hati za makubaliano **20** zilizohusisha masuala ya mifumo, ujenzi wa Hospitali ya Makunduchi, utoaji wa huduma kupitia kambi za matibabu na huduma za dharura. Aidha, Wizara imetia saini Mikataba **30** ya utoaji wa huduma ikiwemo; Ujenzi, dawa, vifaa tiba, mifumo, mafuta, ulinzi, vifaa vya usafi, vifaa vya kuandikia na mafunzo. Vile vile Wizara imeingia mikataba iliyoshirikisha

Taasisi binafsi katika utoaji huduma za Afya (Outsourcing) kama ifuatavyo:

i. Mkataba wa uendeshaji wa huduma, dawa na vifaa tiba kwa Hospitali za Wilaya za Unguja na Pemba na Saifee Hospital Zanzibar Limited;
ii. Mkataba wa uendeshaji wa huduma, Dawa na Vifaa Tiba kwa Hospitali ya Lumumba na NSK Hospital Limited;
iii. Mkataba wa huduma za radiolojia kwa hospitali za Wilaya Unguja na Pemba na NSK Hospital Limited
iv. Mkataba wa utoaji wa huduma za uchunguzi wa kimaabara na radiolojia na LANCET Laboratories Tanzania Limited kwa Hospitali za Wilaya;
v. Mkataba wa huduma za Afya ya Wafanyakazi na ZanzMedical Hospital

## HUDUMA ZA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA

**108. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuratibu shughuli za manunuzi ya Wizara ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya vikao vya zabuni **19** vimefanyika. Vikao hivyo vilijadili zabuni ya Ujenzi wa Nyumba za wafanyakazi kwa Hospitali tano (**5**) za Wilaya za Pangatupu, Mwerapongwe, Kitogani kwa Unguja na Kinyasini na Vitongoji kwa Pemba, Zabuni ya ujenzi wa vituo vya afya tisa (**9**) (vitano (**5**) Unguja na vinne (**4**) Pemba). Aidha, kikao cha kujadili zabuni ya Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**109. Mheshimiwa Spika,** Vikao vya kujadili zabuni za Mradi wa Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto kupitia Mkopo wa Benki ya Dunia vilifanyika ambapo vilihusisha ununuzi wa vifaa tiba, dawa na virutubisho, magari ya kubebea wagonjwa, magari ya kubebea taka na vifaa vya TEHAMA. Aidha, zabuni za Kampuni binafsi za dawa kwa hospitali ya Abdulla Mzee Pemba na uendeshaji wa hospitali ya Lumumba zilijadiliwa. Katika hatua nyengine, zabuni za ununuzi wa chanjo za mahujaji, ununuzi wa vitendanishi na dawa za kupuliza majumbani pamoja na ununuzi wa dawa za malaria zilijadiliwa.

**HUDUMA ZA AFYA KIDIGITALI**

**110. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya katika kuimarisha utoaji wa huduma, imeweza kuweka mfumo wa kidigitali katika hospitali **10** za Wilaya na moja (**1**) ya Mkoa, mfumo huo ni kwa ajili ya kutunza taarifa za matibabu kielektroniki na kufuata mwenendo wa mgonjwa (Patient Journey) tangu anapoingia hospitali mpaka anapotoka na hivyo kuimarisha ufanisi wa utendaji na utoaji wa huduma katika hospitali hizo. Aidha, Wakala wa Bohari kuu ya Dawa imeboresha mfumo wa mSupply ambao unategemewa kutumika kwenye vituo vya afya pamoja na kuonesha taarifa zake kwa kutumia njia ya "Dash-board".

**111. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi inaendesha kazi zake za kila siku kwa mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha na kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Mifumo hiyo ni pamoja na **"Pharmacovigilance System"** mfumo huu ni wa ufuatiliaji usalama wa dawa ambao unajumuisha utambuzi, tathmini, uelewa na udhibiti wa madhara yatokanayo na dawa. Pia mfumo wa **"Clinical Trial System"** Mfumo huu hupokea maombi ya majaribio ya dawa na umeunganishwa na mfumo wa Taasisi ya Utafiti wa Afya (ZAHRI) ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwenye Taasisi hizi mbili ili kudhibiti majaribio ya dawa, na mfumo "**ZFDA web portal"** Huu ni mfumo mkuu wa kutoa vibali na ukaguzi wa maeneo ya biashara, usajili wa bidhaa na uombaji wa vibali vya uingizaji wa bidhaa zinazodhibitiwa na ZFDA.

**112. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ufuatiliaji wa taarifa za afya katika hospitali na vituo vya afya, Wizara imefanikiwa kuimarisha mfumo mama wa taarifa za afya DHIS-2 kutoka version **2.38** na kwenda version **2.40.3.1**. Mfumo huu umeongezewa uwezo wa kusomana na mifumo mengine katika hospitali, vituo vya afya na maeneo mengine ya utoaji wa huduma. Lengo kuu la wizara ni kupunguza utitiri wa mifumo na kuwa na mifumo michache inayosomana na kutoa taarifa kwa wakati ili kuwezesha utoaji wa maamuzi sahihi katika ngazi zote za utoaji wa huduma.

**PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI (SH010302)**

**113. Mheshimiwa Spika,** Program hii ina jukumu la uandaaji wa mipango na bajeti ya sekta, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi za wizara na programu za miradi ya maendeleo, kutayarisha na kuzifanyia mapitio Sera na miongozo pamoja na kuratibu na kufanya tafiti za afya. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii ilitengewa kiasi cha Shilingi **1,449,227,000/=** ambapo hadi kufika Machi 2024 iliingiziwa na kutumia jumla ya Shilingi **551,322,017/=** sawa na asilimia **35.**

**114. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/24 Wizara inaendelea kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo mbali mbali ya utoaji wa huduma. Jumla ya miradi **11** yenye thamani ya Shilingi bilioni **76.8** inatekelezwa kupitia fedha za serikali Shilingi bilioni **54.18** na Shilingi bilioni **22.62** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Mradi wa ujenzi wa vituo vya afya kumi (**10**) upo katika hatua mbali mbali ukiwa na lengo la kuimarisha afya ya msingi kwa kuimarisha miundombinu. Vituo hivyo ni Kizimkazi, Mpendae, Sebleni, Nungwi, Tunguu, Mahonda, Jadida, Konde, Chonga na Mtambile.

**115. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika jitihada za kuimarisha afya ya msingi imefanikiwa kufanya uhakiki wa vituo vyote **172** vya afya matokeo yameonyesha kuwa vituo **142** **(**Unguja **82** na Pemba **60)** vimekidhi vigezo vya kutoa

huduma za afya ya msingi kati ya hivyo Dispesari **90** na Vituo vya Afya **52**. Aidha, jumla ya vituo vya afya **39** vinahitaji kufanyiwa matengenezo madogo, vituo **85** vinahitaji kujengwa upya na jumla ya vituo **18** vinahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa. **Kiambatisho nambari 5a kinafafanua zaidi.**

**116. Mheshimiwa Spika,** wizara kwa mwaka wa fedha ujao 2024/25 imetenga jumla ya Shilingi bilioni **137.1** (Shilingi bilioni **75.0** kutoka Serikalini na Shilingi bilioni **62.1** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) ili kutekeleza miradi ya maendeleo (**9**), miradi (**5**) inalenga kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya  miradi (**4**) ni ya ujenzi wa miundombinu ya afya ikiwemo kuendelea na ujenzi wa vituo vya afya, nyumba za wafanyakazi, Ujenzi wa Hospital ya Mkoa ya Mahonda, ujenzi wa Bohari kuu ya Dawa, Ujenzi wa Ofisi ya Wizara-Pemba na Ukarabati na Ujenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**117. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisa usimamizi na uratibu wa vipaumbele vya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Wizara kupitia Taasisi ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa shughuli Serikalini (PDB) imeweza kuleta mabadiliko na mageuzi kwenye maneo muhimu yakiwemo Bohari Kuu ya dawa, Mfuko wa Huduma za Afya, mashirikiano na Sekta Binafsi (Outsourcing), uwekezaji na kutoa ushauri katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**118. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya Mapitio ya sera ya afya ya mwaka 2011 na kuandaa rasimu ya Sera mpya ya mwaka 2024 ambayo imezingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026 (ZADEP) na Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025. Vile vile, Sera hii imezingatia maudhui ya Sera mbali mbali za Kisekta yanayohusiana na masuala ya afya.

**119. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kudhibiti ubora na viwango vya utoaji wa huduma za afya imefanya ukaguzi katika hospitali na vituo vya afya ambapo jumla ya hospitali **4** na vituo vya afya **258** vilifikiwa na kukaguliwa. Ukaguzi umeonesha kuwa vituo **188** vipo daraja la **1** au nyota moja ya viwango, vituo **58** daraja la **2** na vituo **16** daraja la **3**. Hali halisi imeonyesha bado vituo vyetu havijakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa kimataifa ambapo vituo vinatakiwa viwe na ubora kuanzia daraja au nyota tano (**5**), daraja la nne (**4**) na daraja la tatu (**3**).

**120. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha udhibiti wa taarifa za afya, wizara imetayarisha mungozo wa usimamizi wa upatikanaji wa taarifa za afya (Data Access and Sharing guidelines 2024) wenye lengo la kudhibiti utoaji wa taarifa na matumizi sahihi ya taarifa za afya kwa wadau mbali mbali.

## MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZHSF)

121. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi 2023/2024 Mfuko wa Huduma za Afya (ZHSF), ulikadiria kukusanya Shilingi bilioni **35.75** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kwa kipindi hicho jumla ya Shilingi bilioni **32.28** zilikusanywa sawa na asilimia **90** ya makadirio. Fedha hizo zinajumuisha Shilingi bilioni **30.5** ikiwa ni michango ya wanachama, Shilingi bilioni **1.5** fedha kutoka Serikalini, Shilingi milioni **2.5** Ada ya maombi ya watoa huduma, Shilingi milioni **227.5** mapato yatokanayo na uwekezaji na Shilingi milioni **50** fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo kama msaada wa kitaalamu.

122. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, Mfuko umesajili wanachama **48,929** kutoka Sekta ya Umma ambapo lengo ni kusajili watumishi **57,000** sawa na asilimia **86** ya lengo. Aidha mfuko umesajili wanachama wategemezi **187,641** na kufanya idadi ya wanachama wote wa mfuko kufikia **236,570.**

123. **Mheshimiwa Spika,** mahudhurio ya wagonjwa **78,260** yalisajiliwa katika hospitali za Umma, za Kijeshi na Binafsi. Mahudhurio ya wagonjwa **4,039** yalisajiliwa katika Hospitali za Umma sawa na asilimia **5.2**, mahudhurio **14,113** yalisajiliwa katika hospitali za Kijeshi (Polisi, KVZ, Mafunzo na KMKM) sawa na asilimia **18.03** na mahudhurio **60,108** yalisajiliwa katika hospitali za binafsi sawa na asilimia **76.8**.

124. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ulipaji wa madai Shilingi bilioni **5.00** zilikadiriwa kulipwa. Hadi kufikia Machi, 2024 Shilingi bilioni **4.7** zililipwa, ambapo Shilingi bilioni **3.3** zililipwa NHIF kwa wanachama wa ZHSF wanaopata huduma kupitia NHIF na Shilingi bilioni **1.4** zililipwa kwa watoa Huduma wanaowahudumia wanachama wa ZHSF.

125. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa shughuli za uendeshaji wa Ofisi Shilingi bilioni **1.85** zimetumika ikiwemo kufanya uchapishaji wa fomu za wagonjwa, kulipia kodi ya pango ya Ofisi Unguja na Pemba, Matengenezo ya ofisi, ununuzi wa vifaa na utengenezaji wa mifumo vya TEHAMA na ununuzi wa samani.

126. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ushajihishaji na utoaji wa elimu kwa umma, Mfuko ulipanga kufanya mikutano **144 (**Unguja **80,** Pemba **64**) ya kuhamasisha jamii ambapo lengo ni kufanya mikutano **150** ambayo ni sawa na utelezaji wa asilimia **96**. Mfuko umetoa vipeperushi **1,500**, umefanya vipindi **13** katika vyombo vya habari, umetoa matangazo katika redio na televisheni na kushiriki katika maonyesho ya Kitaifa Unguja na Pemba.

127. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mfuko wa Huduma za Afya, unakadiria kukusanya jumla ya Shilingi bilioni **68.90** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kati ya hizo Shilingi bilioni **67.70** ni michango ya wanachama

na Shilingi bilioni **1.2** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa upande wa matumizi, Mfuko unategemea kutumia Shilingi bilioni **6.645** kwa shughuli za kawaida na maendeleo na Shilingi bilioni **44.9** ni kwa ajili ya ulipaji wa madai. Shilingi bilioni **17.40** kwa ajili ya uwekezaji na Shilingi bilioni **6.60** kwa shughuli za kawaida na maendeleo. Hivyo, kufanya matumizi ya jumla kuwa ni Shilingi bilioni **68.90**.

**128. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mfuko wa Huduma za Afya umepanga kukamilisha usajili wa watumishi wa Sekta binafsi na kusajili wanachama wa sekta isiyo rasmi kwa asilimia **60**, kuwawezesha wanachama wa ZHSF kupata huduma Tanzania Bara kwa kupitia NHIF na kuwekeza katika "Biometric" ili kuwatambua wanachama halisi wanaopata huduma za ZHSF.

**129. Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Mfuko umepanga kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa kuwekeza katika "Artificial Intelligence" ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa shughuli za Mfuko, kuongeza utoaji wa elimu kwa umma ili kuwafikia walengwa wengi zaidi (Taasisi **3,000** za umma na binafsi na makundi ya kijamii **50**), kuhakisha kunawekwa udhibiti mzuri wa huduma za maradhi yasio ambukiza, kuhakikisha Mfuko unatafuta fedha kwa Washirika wa Maendeleo kupitia Wizara ya Fedha ili kugharamia matibabu ya maradhi yasio ambukizwa na kudhibiti vitendo vya udanganyifu kwa kutumia teknolojia za kisasa.

**TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZA BINAADAMU – (ZAHRI)**

**130.** **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya utafiti wa Afya kwa kipindi cha cha Julai 2023-Machi 2024 ilipanga kutumia jumla ya fedha za ruzuku Shilingi **481,500,000/=** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji. Hadi kufikia Machi 2024 Taasisi ilipata jumla ya Shilingi **151,495,800/=** ambayo ni sawa na asilimia **31** ya fedha zilizotengwa.

**131.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia taasisi ya Utafiti wa Afya (ZAHRI) imefanikiwa kufanya "Publication" ya tafiti **3** ambazo ni kujua kinga ya mwili baada ya maradhi ya UVIKO-19 kwa wanafunzi, watu waliokweda sokoni na wafanyakazi wa afya. Watu **720** walishiriki katika utafiti huu Unguja na Pemba ambapo asilimia **33** ya washiriki wenye umri kati ya **40-49** walionesha kuwahi kupata maambukizo ya UVIKO-19 na hasa waliotembelea maeneo ya sokoni ukilinganisha na mashuleni na hospitali. Pia utafiti umeonesha wakaazi wa mjini walipata maambukizi zaidi ya maradhi kuliko wanaoishi vijijini.

**132.** **Mheshimiwa Spika**, Utafiti mwengine unaofanana na huu ulifanyika kwa akina mama **1,082** waliofikia umri wa kujifungua. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa asilimia **83** ya akina mama walipata maambukizi na wameweza kujijengea kinga ya mwili kutokana na maambukizi hayo, ukali wa maradhi na vifo vitokanavyo na

ugonjwa wa UVIKO-19 umeonyesha kuwa wa kiwango cha chini tofauti na nchi jirani na hata ughaibuni. Kiwango cha chanjo ya UVIKO-19 kimeonesha kuwa ni cha chini sana na hii iimetokana na taarifa potofu za chanjo hiyo kwenye jamii. Matokeo ya tafiti hizo yameshawasilishwa kwa wadau katika ngazi tofauti ikiwemo machapisho (Publications) katika majarida ya kimataifa.

**133. Mheshimiwa Spika**, Taasisi imefanikiwa kumaliza mradi wa "ASCEND" ambao ulikua na lengo la kuimarisha mifumo ya kupokea na kusajili tafiti pamoja na kuendeleza kufanya tafiti za "*Clinical trial*". Kwa sasa Taasisi tayari imeshamiliki mfumo huo na imeanza kupokea tafiti kutoka ndani na nje ya nchi kupitia mfumo huo unaoitwa "*Zanzibar Health Research Electronic Information Management System* (ZAHREIMS)". Pia kupitia mradi huo watafiti **8** wamepata mafunzo ya "*Good Clinical Practice*" (GCP) pamoja na mambo yanayohusiana na maadili ya tafiti (Research Ethics), mafunzo ambayo yataweza kusaidia watafiti kufanya tafiti zao kwa kumlinda mwananchi juu ya madhara yatokanayo na tafiti.

**134. MheshimiwaSpika,** Taasisi inaendelea kufanya mashirikiano na Taasisi za ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya tafiti mbili **(2)** zinaendelea kutekelezwa kupitia miradi ya pamoja kama ifuatavyo:

i. Mradi wa kupunguza matumizi ya dawa za Antibiotiki kwa Watoto katika hospitali (*Optimizing the Use of Antibiotics in Childhood Infections in Selected wards of Two Hospitals in Zanzibar*). Mradi huu unafadhiliwa na shirika la *International Centers for Antimicrobial Resistance Stewardship* (ICARS) kwa kiasi cha fedha Shilingi **540,378,347.10/=** kwa muda wa miaka minne kuanzia mwaka 2023 hadi 2026.

ii. Mradi wa mafunzo kwa watafiti (*Clinical Trials and Modernized Online Research Protocol Submission System*) kwa ufadhili wa "*European and Developing Countries Clinical Trials Partnership Programme"* (EDCTP2)" ambapo jumla ya fedha Shilingi **43,000,000/=** zimetengwa kwa muda wa miaka mitatu 2023-2025.

**135. Mheshimiwa Spika**. Kwa mwaka wa fedha 2023/24 Taasisi imefanikiwa kutoa vibali vya maadili ya tafiti za afya **166** kati ya hivyo vibali **127** ni vya wanafunzi na vibali **39** ni kutoka Taasisi za ndani na nje ya nchi. Vile vile, Taasisi imeandaa muongozo unaojulikana "*Adjunct Research Fellow"* ambao itasaidia kuvutia watafiti wabobezi kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuandika miradi ya kitafiti.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA WIZARA YA AFYA PEMBA (SH010303)**

136. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Afya Pemba ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi **22,407,926,000/=** zikijumuisha Shilingi **21,663,426,000/=**kwa ajili ya mishahara, Shilingi **744,500,000**/= kwa kazi nyenginezo.

137. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi 2024, Wizara iliingiziwa na kutumia jumla ya Shilingi **19,409,332,177/=** sawa na asilimia **86.6** ya makadirio ya mwaka 2023/2024. Kati ya hizo Shilingi **16,965,210,341/=** sawa na asilimia **78.3** kwa ajili ya mishahara, Shilingi **575,055,135/=** sawa na asilimia **77.2** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

138. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato, Wizara ya Afya Pemba ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi **142,658,000/=**. Hadi kufikia Machi 2024, Wizara ilikusanya Shilingi **26,215,500/=** sawa na asilimia **18.4** ya fedha zilizokadiriwa.

139. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyengine jumla ya wafanyakazi **51** wameajiriwa hadi kufikia Machi 2023. Miongoni mwao ni Afisa Maabara Msaidizi **6**, Afisa Tabibu **17**, Afisa Usafiri **1**, Mfamasia Msaidizi **8**, Mhandisi **1** na Muuguzi Msaidizi **18.** Aidha wafanyakazi 33 wa kada

mbalimbali wamestaafu na wafanyakazi **2** wamechukua likizo bila malipo katika kipindi hiki. Kwa upande mwengine wafanyakazi **4** wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema Peponi, Amiin.

**140. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekuwa ikiimarisha huduma za afya katika ngazi za msingi kwa kuboresha miundombinu yake ya kutolea huduma. Katika ngazi hii ujenzi wa kituo cha afya (Dispensary) cha Vumba Mchangamdogo kinachojengwa kwa ufadhili wa mradi wa TASAF na Kituo cha Afya cha Minungwini ambacho kinajengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kojani unaendelea.

## PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (FUNGU H02)

**141. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inajumuisha utekelezaji wa Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wazazi Mwembeladu na Hospitali ya Wagonjwa wa Afya ya akili Kidongo Chekundu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **49,772,000,000/=** ikiwa Shilingi **24,372,400,000/=** ni kwa mishahara ya wafanyakazi, Shilingi **14,274,400,000/=** ni kwa kazi za uendeshaji ikiwa ni pamoja na matumizi ya ulipaji wa kampuni za uchunguzi, dawa na vifaa tiba. Kwa upande wa miradi ya maendeleo jumla ya Shilingi **11,125,200,000/=** zilipangwa ambapo Shilingi **1,125,200,000/=** ni mchango kutoka Serikalini kwa Mradi wa kupandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja na Shilingi **10,000,000,000**/= ni kutoka kwa wafadhili wa mradi huo **(BADEA, KUWAIT NA SAUDI)** kwa ajili ya Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**142. Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Shilingi **27,358,992,724.18/=** sawa na asilimia **54.9** ziliingizwa kwa matumizi mbali mbali ambapo Shilingi **16,443,441,399.50/=** kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi na Shilingi **2,326,198,373.58/=** zimetumika kwa uendeshaji wa Hospitali. Aidha, Programu imelipa Shilingi **8,589,352,951.1/=**kwa kampuni ya huduma za uchunguzi na kampuni ya usambazaji dawa na vifaa tiba. **Kiambatisho 1c**.

143. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Shilingi **1,045,951,391/=** sawa na asilimia **93** zimetumika kwa malipo ya ununuzi wa vifaa tiba, mashine za hospitali pamoja na ununuzi wa computer kurahisisha ukusanyaji wa taarifa binafsi za wagonjwa kupitia mfumo wa kielektroniki. Aidha kwa upande wa Washirika wa Maendeleo, Jumla ya Shilingi **970,905,000/=**zimeingizwa kwa malipo ya mshauri muelekezi na mishahara ya wafanyakazi wa mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja (BADEA, Saudi Fund pamoja na Kuwait Fund).

144. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi **1,348,585,000/=** kupitia vyanzo vya malipo ya Huduma za Afya, Huduma za Haraka (Fast Track), huduma za Bima na malipo ya wanafunzi wa kigeni, hadi kufikia Machi, 2024 programu imekusanya jumla ya Shilingi **505,714,452.85/=** sawa na asilimia **37.** Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana kwenye **Kiambatanisho namba 1d.**

145. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa program ndogo za Hospitali ya Mnazi Mmoja kama ifuatavyo; -

## PROGRAM NDOGO YA UCHUNGUZI NA MATIBABU (SH0201)

146. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Programu hii ilitengewa jumla ya Shilingi **4,200,000,000/=** hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Shilingi **3,828,946,068.14/=** zilitumika kwa malipo ya kampuni ya huduma za uchunguzi ambapo sawa na asilimia **91.** Jumla ya vipimo vya maabara **356,834** na vipimo **49,369** kwa njia ya picha (Ultrasound ni **20,261**; X-ray **17,311**, MRI **2,929;** na CT-scan **8,868**) vilifanyika.

147. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za matibabu, programu hii inaendelea kutoa huduma za dharura, huduma za kliniki kwa maradhi maalum kama vile saratani, moyo, afya ya akili, figo, ngozi na nyenginezo. Programu hii ilitengewa jumla ya Shilingi **7,174,801,000/=.** Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya Shilingi **5,759,228,036.89** sawa na asilimia **80** zilitumika.

148. **Mheshimiwa Spika,** huduma za matibabu zimeendelea kutolewa ambapo wagonjwa wa nje **248,497** walitibiwa (Wanaume **104,749** na Wanawake **143,748**) na wagonjwa **11,820** (wanaume **5,049 na** wanawake **6,771**) walilazwa kwa magonjwa tofauti. Vile vile kwa upande wa Hospitali ya Kidongo Chekundu, jumla ya wagonjwa **628** walilazwa kwa matatizo ya afya akili.

149. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, katika huduma za Uzazi, jumla ya wajawazito **14,025** (Mwembeladu **1,992 na** Mnazi Mmoja **12,033**) walipokelewa, kati ya hao wajawazito **7,978** (Mnazi Mmoja-**6,256** na Mwembeladu-**1,722)** walijifungua kwa njia ya kawaida na wajawazito **2,742** walijifungua kwa njia ya Upasuaji.

150. **Mheshimiwa Spika,** Huduma za matibabu ya kusafisha Damu (Dialysis) kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo zimeendelea kutolewa kwa wagonjwa **540** wakiwemo wagonjwa wapya **71.** Aidha, wagonjwa **204** wanapatiwa huduma katika kliniki ya saratani. Katika hatua nyengine, mahudhurio ya wagonjwa **5,225** wamepatiwa matibabu katika kliniki maalumu ya maradhi ya moyo, ambapo wagonjwa **1,267** ni wapya na wagonjwa **3,958** wa marejeo.

151. **Mheshimiwa Spika,** Programu imeendesha kambi za uchunguzi na matibabu kwa mashirikiano na Madaktari Bingwa kutoka Hispania, Uholanzi, Israel na na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (JKCI, MOI, na Macho), Jumla ya kambi **16** zilifanyika na wagonjwa **1,472** walichunguzwa na kupatiwa matibabu. Kati ya hao, wagonjwa **647** walifanyiwa upasuaji wakiwemo wagonjwa **54** kutoka divisheni ya matibabu ya vichwa maji na uti wa mgongo, wagonjwa **70** walifanyiwa upasuaji wa midomo sungura na kesi za kuunguwa na wagonjwa **97** ni wa matatizo ya mifupa.

**152. Mheshimiwa Spika,** Watoto **174** walifanyiwa uchunguzi wa matatizo ya moyo kati ya hao watoto **87** wamebainika na matatizo hayo na wanahitaji kufanyiwa upasuaji nje ya Zanzibar. Aidha, jumla ya watoto **34** tayari wamepatiwa matibabu ya upasuaji huo nchini Israel.

**PROGRAMU NDOGO YA UONGOZI NA UTAWALA (SH0202)**

**153. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wafanyakazi waliopo ni **1,633**, wafanyakazi **26** wamemaliza masomo na kurudi kazini wakiwemo wauguzi-**10** na madaktari bingwa-**16**. Watalamu hao ni wa fani za afya ya akili, mifupa, matatizo ya damu, macho na upasuaji.

**154. Mheshimiwa Spika**, Hospitali ya Mnazi Mmoja ina jukumu la kufundisha na kusimamia wanafunzi wa kada za afya pamoja na kufanya tafiti mbali mbali zinazohusu afya ya binadamu. Hivyo, vyuo vya Afya vya ndani na nje ya Zanzibar, vinaendelea kuleta wanafunzi wake kwa mazoezi ya vitendo. Jumla ya wanafunzi **2,059** (Vyuo vya ndani-**1,855** na Nje ya nchi **204**) wamepokelewa kufanya mazoezi ya vitendo chini ya usimamizi wa wataalamu wetu kwa mujibu wa kada na fani zao. Aidha*,* vibali (**18**) vimetolewa kwa kufanya tafiti ndani ya hospitali. Pia, Jumla ya wafanyakazi **13** kutoka divisheni ya watoto walipatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mashine ya CPAP kwa muda wa mwezi mmoja katika

Hospitali ya Muhimbili- Dar es salaam kwa ufadhili wa Wizara kwa kushirikiana na Chuo kikuu cha Haukeland cha Nchini Norway.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**155. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kupandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja una lengo la kuimarisha huduma katika hospitali rufaa ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya hospitali ikiwa ni pamoja na kufanya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kisasa vya utibabu. Katika kipindi cha utekelezaji hospitali imeweza kufanya malipo ya computer **110** na Satelite Dish kwa ajili ya uendelezaji wa mfumo wa kielektroniki kwenye wodi za wagonjwa pamoja na kufanya malipo ya vifaa tiba vya huduma za masikio, pua na koo pamoja na mashine za kitengo cha mfumo wa mkojo (Urology).

**156. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Mnazi Mmoja inatekeleza Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ambao ni mashirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wafadhili (BADEA, Saudi Fund pamoja na Kuwait Fund) kwa kufanya shughuli mbalimbali zikiwemo za ujenzi na upanuzi wa majengo pamoja na ununuzi wa vifaa vya utibabu. Mshauri Elekezi (Consultant) ameshaanza kazi alizopangiwa ikiwemo kufanya upembuzi yakinifu, michoro na makadirio

ya gharama za ukarabati wa majengo ya zamani na ujenzi wa majengo mapya (BOQ). Mradi upo kwenye hatua ya kutafuta mkandarasi na zabuni imeshatangazwa na wazabuni wanaendelea kuwasilisha maombi ya ujenzi.

157. **Mheshimiwa Spika**, Mradi wa kubadilishana wataalamu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Chuo Kikuu cha Haukeland cha Norway unaendelea vizuri. Kwa sasa wafanyakazi **3** wako nchini Norway kwa kubadilishana wataalamu ili kupata uzoefu zaidi wa utowaji wa huduma bora kwa wagonjwa. Pia mashine na vifaa mbali mbali vimenunuliwa kama vile CPAP, Arterial Blood Gas analyser, Ultrasound na kadhalika kutoka kwa washirika wetu wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland kwa kurahisha na kuimarisha utoawaji wa huduma kwa wagonjwa na kuimarisha utendaji kazi wa Hospitali.

158. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mradi wa kuimarisha huduma za macho (CBM) inaendelea kufanya uchunguzi pamoja na upasuaji wa macho. Mradi huu umeweza kuchunguza wagonjwa **34,304** (Wanaume-**16,242** na Wanawake-**18,062**) wa macho na wenye ulemavu wa macho na kupatiwa huduma za upasuaji pamoja na kupatiwa visaidizi vya ulemavu kama vile visaidizi vya uoni hafifu pamoja na vya kusikia.

## C. CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

159. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imepitia changamoto zifuatazo: -

i. Uhaba wa rasilimali watu wenye sifa kama vile madaktari bingwa, wataalamu wa ganzi na usingizi, wataalamu wa ICU, wahandisi vifaa tiba, wauguzi wenye shahada ya kwanza, Wakaguzi wa kemikali n.k;

ii. Upungufu wa vifaa vya kutendea kazi kama vile PET scan, mashine ya kuchunguzia sumu (LCMS/MS), DR6000 spectrophotometry, MP-AES, mashine ya kuchunguza saratani ya matiti (mammogram);

iii. Uchakavu wa miundombinu ya vituo vya afya ikiwemo majengo, machine na vifaa tiba;

iv. Kuongezeka kwa matumizi wa dawa za asili kutokana na uuzaji holela wa dawa za asili katika maeneo mbali mbali;

v. Lishe duni ya mama na mtoto inayopelekea maradhi na vifo vinavyotokana na uzazi kwa mama na watoto;

vi. Ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza; na

vii. Kutokufikiwa kwa viwango vya ubora kitaifa na kimataifa katika utoaji wa huduma kwa vituo vya afya ambao inapelekea ugumu wa kutekelezwa kwa mfumo wa rufaa.

## HATUA ZA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

160. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa kutekeleza majukumu hayo, wizara imejaribu kuzitatua kama ifuatavyo: -

i. Wizara kuendelea kutoa mafunzo ya fani adimu pamoja na kuajiri wataalamu wenye sifa zinazohitajika;

ii. Kutenga bajeti ya kutosha kukidhi mahitaji ya ununuzi wa mashine, dawa na matengenezo kinga ya vifaa tiba na majengo (*Preventive Maintenance*);

iii. Kuendelea kuelimisha jamii juu ya madhara yatokanayo na matumizi yasiyosahihi ya dawa asili pamoja na kuimarisha udhibiti wa uuzaji wa dawa asili;

iv. Kuimarisha mashirikiano na sekta zisizo za afya katika kutekeleza mkakati wa Lishe wa Kitaifa (*Multi-sectoral Nutrition Action Plan*);

v. Kuendelea kuelimisha jamii umuhimu wa kubadilisha mfumo wa maisha kwa kuweka msisitizo katika ulaji na kufanya mazoezi; na

vi. Kuendelea kuimarisha afya ya msingi ikiwemo kufanya ukarabati, kujenga upya, kuweka wataalamu wenye sifa na vifaa.

## D. MWELEKEO WA BAJETI NA VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

161. **Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2024/25 imezingatia jinsia na usawa kwa makundi yote kwenye jamii (wanawake na wanaume, wasichana na wavulana) kwa kuhakikisha mgawanyo wa rasilimali fedha unatoa fursa sawa kwa wote. Bajeti inayozingatia jinsia ni muhimu kwa haki ya kijinsia na kwa haki ya kifedha. Kwa muktadha huo wizara imetenga jumla ya Shilingi **22,028,335,000** kwa ajili ya kutekeleza afua zinazolenga Jinsia na Usawa sawa na asilimia **0.7** ya bejeti. **Kiambatisho nambari 5b kinafafanua zaidi.**

162. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Wizara ya afya itaelekeza nguvu zake katika kutekeleza vipaumbele ili kuimarisha huduma za afya nchini kama zinavyoonekana kupitia programu husika kama vifuatavyo:

### PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

163. **Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa kupitia programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Wizara imetenga jumla ya Shilingi **100,619,301,000/=** ambazo ni sawa na asilimia **36** ya bajeti ya Wizara kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendelea kudhibiti maambukizi ya VVU kwa kutoa huduma za ushauri nasaha, upimaji na matibabu;
ii. Kuendelea kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu, Ukoma na Homa ya Ini
iii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi wa mama na mtoto;
iv. Kuimarisha huduma za afya ya Mipakani (Bandarini na Viwanja vya ndege);
v. Kuendelea kutoa huduma za uchunguzi na tiba kwa maradhi ya macho katika vituo vya afya, hospitali, maskulini na jamii;
vi. Kuendelea na mikakati ya kupambana na maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza;
vii. Kuimarisha afya ya jamii na mazingira;
viii. Kuendelea kufanya tafiti mbali mbali zitakazotoa matokeo ili kuimarisha huduma za afya katika kupambana na maradhi;
ix. Kuimarisha program za uhamasishaji na kutoa huduma za afya katika ngazi zote; na
x. Kupambana na maradhi ya mripuko na majanga ya kiafya.

## PROGRAMU YA TIBA

164. **Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha kwamba huduma za uchunguzi na matibabu zinaimarika zaidi, Wizara imetenga Shilingi **142,253,383,000/=** sawa na asilimia **50** kati ya hizo Shilingi **136,331,183,000/=** kwa ajili ya program ya

matibabu na Shilingi **5,922,200,000/=** kwa ajili ya program ya Uchunguzi. Shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa: -

i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu katika hospitali za wilaya na mkoa;
ii. Kutekeleza mfumo wa rufaa kwa wagonjwa katika ngazi zote za utoaji wa huduma;
iii. Kuimarisha kambi za matibabu na mashirikiano ya huduma za afya kimataifa;
iv. Kuongeza ukusanyaji wa damu uniti **25,000** kwa mwaka kutoka uniti **20,000**;
v. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa, tiba na vitendanishi;
vi. Kuimarisha huduma za uchunguzi (maabara na rediolojia);
vii. Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za Afya;
viii. Kuimarisha usimamizi katika uhifadhi na utumiaji wa dawa na vifaa vya utibabu katika hospitali na vituo vya afya;
ix. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa wahanga wa udhalilishaji;
x. Kuimarisha uratibu wa huduma za uuguzi na ukunga; na
xi. Kuimarisha huduma za tiba kwa mashirikiano na sekta binafsi.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA (PHO103)

**165. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, program imetenga Shilingi **39,883,789,000/=** sawa na asilimia **14** kwa ajili ya kutekeleza shughuli kuu zilizopangwa katika programu hii, ambapo Shilingi **2,093,456,000/=** zitatumika kwa shughuli za uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti, Shilingi **10,195,229,000/=** kwa ajili ya Utumishi na Uendeshaji, Shilingi **2,070,100,000/=** kwa ya Taasisi ya Utafiti. Aidha Wizara imetenga Shilingi **25,525,004,000/=** kwa ajili ya Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Afya Pemba. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa kuajiri wataalamu wenye sifa na kupeleka masomoni madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

ii. Kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa sera, sheria, na miongozo ya utoaji huduma za afya;

iii. Kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wa kugharamia huduma za afya;

iv. Kufanya tafiti, ufuatiliaji na tathmini katika ngazi zote za utoaji wa huduma;

v. Kuimarisha mifumo ya kidigitali ya taarifa za afya; na

vi. Kuimarisha miundombinu ya huduma za afya ikiwemo matengenezo ya majengo na vyombo vya usafiri.

**PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (HO2)**

166. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya Shilingi **61,329,600,000/=** zimepangwa kutumika kwa hospitali ya Mnazi Mmoja. Kati ya hizo Shilingi **23,069,600,000/=** zimetengwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi **15,260,000,000/=**kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa hospitali zikiwemo huduma za uchunguzi na matibabu. Aidha, miradi ya maendeleo imepangiwa Shilingi **23,000,000,000/=** kati ya fedha hizo Shilingi **2,000,000,000/=** kutoka Serikalini kwa ajili ya ukarabati na utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Shilingi **21,000,000,000** ni Mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo (BADEA, KUWAIT NA SAUDI FUND).

167. **Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na:

i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi kwa wagonjwa kwa mashirikiano na sekta binafsi pamoja na upatikanaji wa huduma za matibabu ya rufaa

ii. Kuendelea kutoa huduma za kibingwa ikiwemo usafishaji damu kwa wagonjwa zikiwemo huduma za figo, uchunguzi wa saratani (biopsy), matibabu ya satarani (Chemotherapy), huduma za ubongo na uti wa mgongo

iii. Uimarishaji wa kambi maalum za matibabu na kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani

iv. Kuratibu na kufanya tafiti za maradhi mbalimbali

v. Kuongeza ajira kwa wataalamu wakiwemo wataalamu bingwa na wabobezi

vi. Kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi taarifa za wagonjwa (Electronic Medical Record EMR); na

vii. Kuanza ukarabati na utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kupitia mradi wa BADEA, Saudi na Kuwait fund

## E. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**168. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imejipangia kutekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya ikiwemo matengenezo ya majengo na vyombo vya usafiri;

ii. Kuhakikisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na vitendanishi;

iii. Kuimarisha mifumo ya kidigitali ya taarifa za afya;

iv. Kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa kuajiri wataalamu wenye sifa na kupeleka masomoni madaktari na wafanyakazi wa kada nyengine za afya;

v. Kuimarisha mifumo endelevu ya kugharamia huduma za afya ikiwemo mfuko wa afya Zanzibar;

vi. Kuimarisha huduma za afya ya msingi kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

vii. Kupunguza vifo vya mama wajawazito kutoka vifo **145** kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwa 2023/2024 kufika vifo **123** kwa kila vizazi hai 100,000 (Zanzibar Vision 2050) na kufikia vifo 70 kwa kwa kila vizazi hai 100,000 (SDG-2030) ifikapo 2030.

viii. Kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo **28** kwa kila vizazi hai 1000 na kufikia vifo **26** kwa kila vizazi hai 1000 (Zanzibar Vision 2050) na hadi kufikia vifo **12** kwa kila vizazi hai 1000 (SDG-2030) ifikapo 2030;

ix. Kuimarisha uwezo na utayari wa kukabiliana na majanga ya mripuko na matukio mengine ya kiafya;

x. Kuendeleza mapambano ya maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza; na

xi. Kuongeza idadi ya tafiti za afya kwa kuzingatia ajenda za nchi na kufanya uchambuzi wa tafiti hizo kwa lengo kutunga sera na miongozo ili kuimarisha huduma.

## F. SHUKRANI

**169. Mheshimiwa Spika,** kwa kipekee naomba kuchukua fursa hii ya kuwashikuru viongozi mbalimbali wa Wizara ya Afya kwani mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaomalizika ni kutokana na mashirikiano makubwa ninayoyapata kutoka kwa viongozi wenzangu ndani ya wizara akiwemo **Mhe. Hassan Khamis Hafidh** Naibu Waziri wa Afya, Katibu Mkuu **Dkt. Habiba Hassan Omar,** Mkurugenzi Mkuu **Dkt. Amour Suleiman Mohamed**, Afisa Mdahmini Wizara ya Afya Pemba Nd. **Khamis Bilali Ali,** pamoja na Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Divisheni na Vitengo vilivyo chini ya Wizara ya Afya. Aidha, kwa dhati kabisa nawashukuru watendaji wengine wote wa Wizara ya Afya kuanzia ngazi ya jamii, Vituo vya Afya, Hospitali, programu na vitengo vyote kwa kujituma kwa moyo katika kuwahudumia wananchi.

**170. Mheshimiwa Spika,** sasa naomba uniruhusu kuyashukuru Mashirika mbali mbali ya Maendeleo yakiwemo Shirika la Afya la Ulimwenguni - WHO, UNICEF, UNFPA, UNAIDS, UNDP, Jumuia ya Afrika Mashariki, Haukeland University Hospital ya Norway, SAVE THE CHILDREN, Engender Health, D-Tree International, World Diabetic Foundation, World Bank, CDC, AMREF, ICAP, MDH, Sight Saver, HIPZ, USAID, PharmaAcess, Mfuko wa kupambana na UKIMWI, Kifua

Kikuu na Malaria (GFATM), GIZ, Mfuko wa Rais wa Marekani (PMI), THPS, DFID, JHPU, IHI, JICA, PEPFAR, NOAH, Benjamin Mkapa Foundation, Tonny Blair Institute, Zanzibar Maisha Bora Foundation, WAJAMAMA, ZOP na Zanzibar Milele Foundation. Aidha napenda kuzishukuru nchi rafiki kwa mashirikiano yao zikiwemo, Jamhuri ya watu wa China, Serikali ya Cuba, Spain, Canada, Israel, Norway, Ujerumani, Korea, Uturuki, India, Kuwait, Marekani, Italy, Saudi Arabia, Oman, UAE, Uingereza. Aidha, tunatoa shukrani kwa Wizara zote za SMZ pamoja na sekta mbali mbali za Serikali na Binafsi. Sekta hizi zimesaidia sana kwa namna moja ama nyengine katika kuhakikisha jamii inapata huduma za afya kwa wote.

## G. HITIMISHO

### MAOMBI YA FEDHA KWA UTEKELEZAJI WA KAZI ZILIZOPANGWA KWA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**171. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Afya (Fungu H01) inakadiriwa kutumia kiasi cha Shilingi **282,756,472,000/=** Kati ya hizo Shilingi **71,599,300,000/=** kwa ajili ya mishahara, Shilingi **74,056,499,000/=** kwa matumizi mengineyo na Shilingi **7,992,300,000/=** ni Ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara. **Kiambatisho nambari 6a kinafafanua zaidi.**

**172. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kazi za maendeleo, Wizara imepangiwa kutumia Shilingi **129,108,374,000/=** kati ya hizo, Shilingi **73,000,000,000/=** kutoka serikalini na Shilingi **56,108,374,000/=** kati ya hizo Shilingi **16,546,880,000/=** ni msaada na Shilingi **39,561,494,000/= ni** mkopo kutoka kwa mashirika ya maendeleo.

**173. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Mnazi Mmoja Fungu (H02) imepangiwa kutumia Shilingi **61,329,600,000/=** kati ya hizo Shilingi **23,069,600,000/=** kwa ajili ya mishahara na Shilingi **15,260,000,000/=**kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa hospitali na Shilingi **23,000,000,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati

ya hizo Shilingi **2,000,000,000/=** kutoka serikalini na Shilingi **21,000,000,000/=** ni mkopo kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**174. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato, wizara (Fungu H01) imepangiwa kukusanya Shilingi **3,719,683,000/=** kwa ajili ya kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali. Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02) imepangiwa kukusanya Shilingi **1,339,086,000/=** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. **Kiambatisho nambari 6b kinafafanua zaidi.**

**175. Mheshimiwa Spika,** sasa naomba Wajumbe wa kamati yako waijadili hotuba hii na hatimae waridhie matumizi ya Shilingi **282,756,472,000/=** kwa Wizara ya Afya (Fungu H01) na Shilingi **61,329,600,000/=** kwa matumizi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja (Fungu H02). Aidha, waridhie makusanyo ya Shilingi **3,719,683,000/=** kwa Wizara ya Afya na Shilingi **1,339,086,000/=** kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**176. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.



**.........................................**

**NASSOR AHMED MAZRUI (MBLW)**

**WAZIRI WA AFYA,**

**ZANZIBAR.**

## *Kiambatisho Namba 1a:* UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2023/24 KWA KIPINDI JULAI HADI MARCH 2024

| HUDUMA | PROGRAMU | BAJETI 2023/24 | MAKADIRIO YA BAJETI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI 2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA KIPINDI CHA JULAI MACH 2024 | % | % YA MAKADIRIO YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MSHAHARA | KINGA | 22,225,852,920 | 16,669,389,690 | 17,665,754,506.00 | 105.98 | 79.48 |
| | TIBA | 9,261,482,600 | 6,946,111,950 | 11,438,446,932.00 | 164.67 | 123.51 |
| | UTUMISHI | 5,388,945,520.00 | 4,041,709,140 | 3,251,814,378 | 80.46 | 60.34 |
| | MIPANGO NA UTAFITI | 1,474,092,960.00 | 1,105,569,720 | 1,418,320,434.00 | 128.29 | 96.22 |
| | URATIBU WA SHUGHULI ZA AFYA PEMBA | 21,663,426,000.00 | 16,247,569,500 | 16,965,210,341 | 104.42 | 78.31 |
| | **JUMLA YA MSHAHARA** | **60,013,800,000.00** | **45,010,350,000.00** | **50,739,546,591.00** | **112.73** | **84.55** |
| **HUDUMA** | | | | | | |
| OC | KINGA | 3,698,371,600.00 | 2,773,778,700 | 493,637,780.00 | 17.80 | 13.35 |
| | TIBA | 40,727,432,080.00 | 30,545,574,060 | 24,145,279,687.71 | 79.05 | 59.29 |
| | UTUMISHI | 4,489,157,940.00 | 3,366,868,455 | 3,078,821,356.00 | 91.44 | 68.58 |
| | MIPANGO | 1,191,505,040.00 | 893,628,780 | 1,237,096,261.00 | 138.44 | 103.83 |
| | URATIBU WA SHUGHULI ZA AFYA PEMBA | 8,520,619,340.00 | 6,390,464,505 | 1,780,000,000.00 | 27.85 | 20.89 |
| | **JUMLA YA OC** | **58,627,086,000.00** | **43,970,314,500.00** | **30,734,835,084.71** | **69.90** | **52.42** |
| **RUZUKU** | | | | | | |
| MSHAHARA | BODI YA CHAKULA NA DAWA -UNGUJA | 1,761,984,484.00 | 1,321,488,363 | 1,680,996,177.00 | 127.20 | 95.40 |
| | MAABARA YA MKEMIA MKUU-UNGUJA | 1,019,036,568.00 | 764,277,426 | 973,871,126.00 | 127.42 | 95.57 |
| | BODI YA CHAKULA NA DAWA-PEMBA | 376,600,500.00 | 282,450,375 | 368,416,830.00 | 130.44 | 97.83 |
| | MAABARA YA MKEMIA MKUU-PEMBA | 173,676,908.00 | 130,257,681 | 195,405,004.00 | 150.01 | 112.51 |
| | **JUMLA** | **3,331,298,460.00** | **2,498,473,845.00** | **3,218,689,137.00** | **128.83** | 96.62 |
| **RUZUKU** | | | | | | |
| OC | BODI YA CHAKULA NA DAWA -UNGUJA | 200,000,000.00 | 150,000,000 | 107,683,000.00 | 71.79 | 53.84 |
| | MAABARA YA MKEMIA MKUU-UNGUJA | 799,800,000.00 | 599,850,000 | 397,101,836.00 | 66.20 | 49.65 |
| | BODI YA CHAKULA NA DAWA-PEMBA | 100,000,000.00 | 75,000,000 | 41,619,000.00 | 55.49 | 41.62 |
| | MAABARA YA MKEMIA MKUU-PEMBA | 150,000,000.00 | 112,500,000 | 58,681,000.00 | 52.16 | 39.12 |
| | TAASISI YA UTAFITI | 481,500,000.00 | 361,125,000 | 171,100,000.00 | 47.38 | 35.53 |
| | **JUMLA** | **1,731,300,000.00** | **1,298,475,000.00** | **776,184,836.00** | **59.78** | **44.83** |
| | | **5,062,598,460.00** | **3,796,948,845.00** | **3,994,873,973.00** | **188.60** | **141.45** |
| **MRADI YA MAENDELEO** | SMZ FEDHA ZA NDANI | 53,050,000,000.00 | 39,787,500,000 | 22,282,784,759.00 | 56.00 | 42.00 |
| | WASHIRIKA WA MAENDELEO | 10,836,278,940.00 | 8,127,209,205 | 3,100,897,945.00 | 38.15 | 28.62 |
| | MKOPO KUTOKA KWA WASHIRIKA WA MAENDELEO | 1,789,672,600.00 | 1,789,672,600 | 1,557,336,392.87 | 87.02 | 87.02 |
| | **JUMLA WASHIRIKA WA MAENDELEO** | **12,625,951,540.00** | **9,916,881,805.00** | **4,658,234,337.87** | **125.17** | **115.63** |
| | **JUMLA KUU MIRADI YA MAENDELEO** | **65,675,951,540.00** | **49,704,381,805.00** | **26,941,019,096.87** | **54.20** | 41.02 |
| **JUMLA KUU** | | **189,379,436,000.00** | **142,481,995,150.00** | **112,410,274,745.58** | **78.89** | **59.36** |

***Kiambatisho Namba 1b:*** **UTEKELEZAJI WA BAJETI YA HOSPITALI YA MNAZIMMOJA 2023/2024**

| SN | MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA | MAKADIRIO | MAKADIRIO YA MIEZI TISA | MATUMIZI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mshahara | 24,372,400,000 | 18,279,300,000 | 16,453,275,000 | 90.0 |
| 2 | Matumiziya uendeshaji | 14,274,400,000 | 10,425,000,000 | 11,140,000,000 | 106.9 |
| | **JUMLA KUU YA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA** | **38,646,800,000** | **28,704,300,000** | **27,593,275,000** | **96** |
| **SN** | **MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO** | **MAKADIRIO** | **MAKADIRIO YA MIEZI TISA** | **MATUMIZI** | **ASILIMIA** |
| 1 | Fedha za Ndani (SMZ) | 1,125,200,000 | 843,900,000 | 1,045,951,391 | 123.9 |
| 2 | Washirika wa Maendeleo | 10,000,000,000 | 7,500,000,000 | 970,905,000 | 12.9 |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO** | **11,125,200,000** | **8,343,900,000** | **2,016,856,391** | **24** |
| | **JUMLA KUU YA MATUMIZI** | **49,772,000,000** | **37,048,200,000** | **29,610,131,391** | **79.9** |

## *Kiambatisho Namba 1c:* MUHTASARI WA MAKUSANYO YA WIZARA YA AFYA KUANZIA JULAI 2023 HADI MACHI 2024

| Kifungu | Kasma | Maelezo | Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka 2023/24 | Makadirio ya Makusanyo Julai 2023 hadi Machi, 2024 | Makusanyo Julai hadi Machi 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **H0101** | | **Ofisi Kuu Pemba** | | | | |
| | 1422051 | Huduma za Uchunguzi wa Afya | 142,658,000 | 106,993,500 | 25,610,000 | 24 |
| | | **Jumla Ndogo** | **142,658,000** | **106,993,500** | **25,610,000** | **24** |
| | | Chief government Chemistry (MKEMIA MKUU) | | | | |
| **H0103** | 1422015 | Huduma za Maabara | 749,981,000 | 562,485,750 | 515,838,412 | 92 |
| | | **Jumla Ndogo** | **749,981,000** | **562,485,750** | **515,838,412** | **92** |
| **H0104** | | **Programa ya Kinga na Elimu ya Afya (PH0101)** | | | | |
| | 1422035 | Shahada ya Maradhi ya kuambukiza | 596,000,000 | 447,000,000 | 66,440,262 | 15 |
| | 1422050 | Huduma za Daktari na orodha ya Wafanyakazi na Abiria | 90,000,000 | 67,500,000 | 58,710,009 | 87 |
| | 1422051 | Huduma za uchunguzi wa Afya | 1,370,000,000 | 1,027,500,000 | 881,843,242 | 86 |
| | 1422078 | Ukodishwajiwa wa Maeneo ya Kibiashara | 30,000,000 | 22,500,000 | 7,350,000 | 33 |
| | 1422124 | Mapato ya UVIKO 19 | 2,000,583,000 | 1,500,437,250 | 194,300,561 | 13 |
| | | **Jumla Ndogo** | **4,086,583,000** | **3,064,937,250** | **1,208,644,074** | **39** |
| **HO105** | | **Program ya Tiba (PH0102)** | | | | |
| | 1422095 | Ada ya Usajili wa Tiba Asili | 132,659,000 | 99,494,250 | 17,324,000 | 17 |
| | | **Jumla Ndogo** | **132,659,000** | **99,494,250** | **17,324,000** | **17** |
| **HO112** | | **Taasisi ya Utafiti wa Afya** | - | | | |
| | 1422094 | Mapato ya Utafiti | 100,000,000 | 75,000,000 | 29,959,620 | 40 |
| | | **Jumla Ndogo** | **100,000,000** | **75,000,000** | **29,959,620** | **40** |
| **HO113** | | **Baraza la Wauguzi** | | | | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Wauguzi | 120,000,000 | 90,000,000 | 55,629,110 | 62 |
| | | **Jumla Ndogo** | **120,000,000** | **90,000,000** | **55,629,110** | **62** |
| **HO114** | | **Baraza la Madaktari** | | | | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Madaktari | 160,000,000 | 120,000,000 | 166,070,987 | 138 |
| | | **Jumla Ndogo** | **160,000,000** | **120,000,000** | **166,070,987** | **138** |
| **H0115** | | **Baraza la Mazingira** | | | | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni wataalamu wa Afya ya Mazingira | 50,000,000 | 37,500,000 | 6,650,500 | 18 |
| | | **Jumla Ndogo** | **50,000,000** | **37,500,000** | **6,650,500** | **18** |
| **H0116** | | **Bodi ya Hospitali Binafsi** | | | | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni kwa Huduma Hospitali Binafsi | 130,000,000 | 97,500,000 | 86,918,180 | 89 |
| | | **Jumla Ndogo** | **130,000,000** | **97,500,000** | **86,918,180** | **89** |
| **H0117** | | **Baraza la Wataalamu wa Maabara** | | | | |
| | 1422119 | Usajili na Leseni Wataalamu wa Maabara | 80,000,000 | 60,000,000 | 42,203,474 | 70 |
| | | **Jumla Ndogo** | **80,000,000** | **60,000,000** | **42,203,474** | **70** |
| **JUMLA KUU KWA FUNGU H01** | | | **5,751,881,000** | **4,313,910,750** | **2,154,848,357** | **50** |

**_Kiambatisho Namba 1d:_ MAKUSANYO JULAI, 2023 HADI MACHI, 2024 KWA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA**

| Maelezo | Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka 2023/2024 | Makadirio ya Makusanyo Julai, 2023 hadi Machi, 2024 | Makusanyo Julai, 2023 hadi Machi, 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Huduma za Uchunguzi na Matibabu** | | | | |
| Malipo ya Huduma za Afya kwa Wagonjwa wenye BIMA | 790,400,000.00 | 593,900,000.00 | 202,768,304.60 | 34.1 |
| Kitengo cha Huduma za Haraka | 300,000,000.00 | 225,000,000.00 | 123,243,297.80 | 54.8 |
| **Jumla ndogo** | **1,090,400,000** | **818,900,000** | **326,011,602** | **39.8** |
| **Kitengo cha Uongozi na Utawala** | | | | |
| Ukodishaji wa Maeneo ya Kiabiashara | 8,200,000.00 | 6,147,000.00 | 3,450,000.00 | 56.1 |
| Mapato ya Utafiti | 249,985,000.00 | 187,488,500.00 | 176,252,850.45 | 94.0 |
| **Jumla ndogo** | **258,185,000** | **193,635,500** | **179,702,850** | **92.8** |
| **Jumla Kuu** | **1,348,585,000.00** | **1,012,535,500.00** | **505,714,452.85** | **49.9** |

## *Kiambatisho Namba 2a:* IDADI YA AKINAMAMA WALIOJIFUNGUA VIFO PAMOJA NA VICHANGA VILIVYOFARIKI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI 2024

| Wilaya | Idadi ya kina mama waliojifungulia katika vituo na hospitali | Idadi ya kina mama walijifungulia kwa njia ya upasuaji | Jumla ya watoto walizaliwa hai | Vifo vya kina mama vitokanavyo na uzazi | Vichanga vilivyofariki |
|---|---|---|---|---|---|
| Chakechake | 4,056 | 483 | 4,054 | 7 | 157 |
| Micheweni | 3,261 | 252 | 3,263 | 4 | 89 |
| Mkoani | 2,547 | 230 | 2,561 | 9 | 61 |
| Wete | 2,958 | 361 | 2,978 | 2 | 73 |
| **Jumla Ndogo Pemba** | **12,822** | **1,326** | **12,856** | **22** | **380** |
| Kaskazini A | 4,090 | 389 | 4,137 | 3 | 140 |
| Kaskazini B | 519 | - | 520 | - | 7 |
| Kati | 1,595 | 9 | 1,638 | - | 26 |
| Kusini | 1,372 | 132 | 1,387 | - | 31 |
| Magharibi A | 2,412 | 179 | 2,385 | - | 17 |
| Magharibi B | 3,737 | 215 | 3,717 | - | 62 |
| Mjini | 14,582 | 3,112 | 14,582 | 35 | 755 |
| **Jumla Ndogo Unguja** | **28,307** | **4,036** | **28,366** | **38** | **1,038** |
| **Jumla Kuu** | **41,129** | **5,362** | **41,222** | **60** | **1,418** |

## *Kiambatisho Namba 2a:* KIWANGO CHA CHANJO KIWILAYA - MWAKA 2023

| Wilaya | Chanjo ya Kukinga Ugonjwa wa kifua kikuu(BCG) | Chanjo ya Kukinga Ugonjwa wa Kifaduro, Pepo punda, Degedege, Uti wa Mgongo na Homa ya ini (Penta3) | Chanjo ya Kukinga Ugonjwa wa PepoPunda kwa vijana wa Kike Wenye Umri wa Kuzaa | Chanjo ya Kukinga Ugonjwa wa PepoPunda (TT2+) kwa mama wajawazito | Chanjo ya Kukinga Ugonjwa wa Surua (Measles) | Waliokamilisha chanjo | Chanjo ya Kujikinga na shingo ya kizazi (HPV Vaccine) kwa vijana wa kike wa miaka 9-14 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Chakechake | 94 | 100.4 | 0.45 | 43.5 | 86.7 | 83.2 | 67.5 |
| Mkoani | 111.5 | 89.9 | 1.3 | 38.9 | 93.1 | 106.2 | 61.6 |
| Wete | 92 | 89.3 | 3.9 | 43.5 | 88.2 | 93.9 | 59.7 |
| Micheweni | 98.1 | 89.4 | 0.92 | 44.2 | 84.4 | 78.8 | 95.8 |
| Kaskazini A | 133.3 | 104.9 | 4.8 | 8.7 | 113.8 | 111.5 | 86 |
| Kaskazini B | 82.1 | 86 | 1.3 | 32.2 | 70.4 | 68.6 | 69.2 |
| Kati | 122.2 | 103.3 | 7.6 | 59.3 | 106.4 | 111.9 | 83.5 |
| Kusini | 191.4 | 186.7 | 16.8 | 43.7 | 180.7 | 191.4 | 193.3 |
| Magharibi A | 108 | 75.8 | 0.22 | 69.3 | 93.5 | 103.6 | 49.3 |
| Magharibi B | 119.1 | 86.4 | 4.1 | 53.6 | 98.3 | 102.3 | 52.1 |
| Mjini | 189.3 | 91.2 | 4.3 | 56.9 | 100.5 | 100.4 | 32.2 |
| **Zanzibar** | **118.7** | **91.2** | **2.9** | **38.5** | **95.2** | **98.3** | **62.8** |

*Kiambatisho Namba 3a:* **IDADI YA WAGONJWA WALIOHUDHURIA HOSPITALI WAGOJWA WA NJE NA WALIOLAZWA NA KUFARIKI KWA KIPINDI CHA JUALI 2023 HADI MACHI 2024**

| Hospital | Wagonjwa wa nje | | Wagonjwa waliolazwa | | Waliofariki | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | W'me | W'ke | W'me | W'ke |
| Abdalla Mzee Regional Hospital | 3473 | 4903 | 1,599 | 1,143 | 105 | 76 |
| Chakechake District Hospital | 6,098 | 7,285 | 117 | 304 | 11 | 7 |
| Micheweni District Hospital | 6,653 | 11,814 | 792 | 1,087 | 39 | 24 |
| Kinyasini District Hospital | 12766 | 20461 | 448 | 506 | 20 | 15 |
| Vitongoji Cottage Hospital | 8,640 | 15,082 | 593 | 731 | 33 | 31 |
| Wete District Hospital | 5,957 | 7,957 | 1,142 | 1,313 | 40 | 30 |
| **Jumla Ndogo** | **43,587** | **67,502** | **4,691** | **5,084** | **248** | **183** |
| Chumbuni District Hospital | 22,091 | 39,418 | 340 | 534 | 3 | 2 |
| Kitogani District Hospital | 4,256 | 5,698 | 280 | 457 | 3 | 1 |
| Kivunge District Hospital | 10,795 | 19,685 | 1,271 | 1,640 | 51 | 44 |
| Ijitimai District Hospital | 20,461 | 34,269 | 872 | 1,095 | 7 | 7 |
| Makunduchi District Hospital | 6,701 | 12,655 | 317 | 463 | 3 | 1 |
| Mbuzini District Hospital | 11,050 | 15,681 | - | 35 | 6 | 3 |
| Mwera Pongwe District Hospital | 7,468 | 12,690 | 127 | 233 | 1 | 2 |
| **Jumla Ndogo** | **82,822** | **140,096** | **3,207** | **4,457** | **74** | **60** |
| Al-Rahma Hospital | 3,319 | 4,191 | 671 | 679 | 7 | 4 |
| Tasakhtaa Global Hospital | 6,474 | 7,317 | 334 | 643 | 21 | 19 |
| Tawaqal Hospital | 4,491 | 6,657 | 110 | 393 | 1 | 0 |
| KMKM Kibweni Hospital | 19,748 | 20,394 | 1,026 | 930 | 7 | 8 |
| **Jumla Ndogo** | **34,032** | **38,559** | **2,141** | **2,645** | **36** | **31** |
| **Jumla Kuu** | **160,441** | **246,157** | **10,039** | **12,186** | **358** | **274** |

*Kiambatisho Namba 3b:* **IDADI YA WAGOJWA WALIOHUDHURIA KLINIKI KWA KIPINDI JULAI 2023 HADI MACHI 2024**

| Kliniki Maalum | W'me | W'ke | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Accupunture | 693 | 1,411 | 2,104 |
| Cardiac | 2,563 | 3,785 | 6,348 |
| CTC | 971 | 1,442 | 2,413 |
| Dental | 6,614 | 9,335 | 15,949 |
| Diabetic | 1,921 | 2,540 | 4,461 |
| ENT | 3,552 | 1,597 | 5,149 |
| Eye | 5,674 | 6,840 | 12,514 |
| Eye Theatre | 320 | 317 | 637 |
| Gynacology | - | 5,886 | 5,886 |
| Major Theatre | 1,112 | 822 | 1,934 |
| Oncology | 536 | 1,108 | 1,644 |
| Orthopedic | 137 | 185 | 322 |
| Physiotherapy | 4,443 | 6,159 | 10,602 |
| Psychatric | 2,147 | 2,707 | 4,854 |
| STI | 935 | 7 | 942 |
| Surgical OPD | 3,475 | 3,050 | 6,525 |
| Utra Sound | 1,005 | 10,357 | 11,362 |
| X-ray | 3,092 | 2,676 | 5,768 |
| **JUMLA** | **39,190** | **60,224** | **99,414** |

*Kiambatisho Namba 3c:* **IDADI YA WAGOJWA WALIOPATIWA HUDUMA ZA VIPIMO KWA KIPINDI JULAI 2023 HADI MACHI 2024**

| Hospital | Vipimo vya Maabara | Vipimo vilivyotolewa kwa njia ya Picha | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | X-ray | Ultra Sound | CT Scan | ECG |
| Kivunge | 65,994 | 4,117 | 5,633 | 0 | 0 |
| Makunduchi | 17,182 | 904 | 3,131 | 0 | 0 |
| Abdallah Mzee | 73,977 | 4,872 | 7,989 | 1,989 | 50 |
| Wete | 10,476 | 687 | 2,236 | 0 | 0 |
| ChakeChake | 32,017 | 376 | 6,325 | 0 | 0 |
| Micheweni | 44,830 | 620 | 5,079 | 0 | 0 |
| Vitongoji | 56,022 | - | 1,410 | 0 | 0 |
| Ijitimai | 67,809 | 5,112 | 9,715 | 0 | 0 |
| Kitogani | 38,706 | 55 | 4,276 | 0 | 0 |
| Chumbuni | 64,330 | 2,593 | 7,584 | 0 | 0 |
| Mbuzini | 25,939 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mwera Pongwe | 19,424 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kinyasini | 28,595 | 1,433 | 3,961 | 0 | 0 |
| Panga tupu | 11,088 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla ya Wote** | **556,389** | **20,769** | **57,339** | **1,989** | **50** |

*Kiambatisho Namba 3d:* **IDADI YA WAGONJWA WALIOTIBIWA NJE YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024**

| S/N | JINA LA HOSPITALI | NCHI | W'me | W'ke | IDADI YA WAGONJWA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Muhimbili Orthopedic Insitute | Tanzania Bara | 69 | 24 | 93 |
| 2 | Jakaya Kikwete Cardiac Institute | Tanzania Bara | 41 | 22 | 63 |
| 3 | Muhimbili National Hospitali | Tanzania Bara | 43 | 40 | 83 |
| 4 | Ocean Road Cancer Institute | Tanzania Bara | 8 | 22 | 30 |
| 5 | MIOT | INDIA | 30 | 36 | 66 |
| 6 | KCMC | Tanzania Bara | 26 | 14 | 40 |
| **JUMLA** | | | **217** | **158** | **375** |

***Kiambatisho Namba 3e:*** **IDADI YA WATEJA WA MATUKIO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024**

| Matukio ya udhalilishaji | Unguja | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 0-4 Miaka | 5-9 Miaka | 9 -14 Miaka | 15-19 Miaka | 20-24 Miaka | 25-59 Miaka | 60+ Miaka | Jumla ya Wote |
| Udhalilishaji wa kimwili | 5 | 13 | 7 | 1 | 0 | 0 | 1 | 27 |
| Udhalilishaji wa kingono | 17 | 68 | 119 | 211 | 8 | 34 | 0 | 457 |
| Udhalilishaji wa kihisia | 2 | 3 | 12 | 33 | 70 | 238 | 4 | 362 |
| Ujauzito | 1 | 12 | 3 | 77 | 10 | 6 | 0 | 109 |
| Kulawitiwa | 17 | 18 | 87 | 197 | 12 | 17 | 0 | 348 |
| Jaribio la kubakwa na kulawitiwa | 8 | 12 | 13 | 2 | 0 | 0 | 1 | 36 |
| Kulawitiwa | 63 | 151 | 264 | 441 | 22 | 28 | 2 | 971 |

| Matukio ya udhalilishaji | Pemba | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 0-4- Miaka | 5-9 Miaka | 9 -14 Miaka | 15-19 Miaka | 20-24 Miaka | 25-59 Miaka | 60+ Miaka | Jumla ya Wote |
| Udhalilishaji wa kimwili | 3 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 |
| Udhalilishaji wa kingono | 9 | 8 | 21 | 34 | 5 | 3 | 0 | 80 |
| Udhalilishaji wa kihisia | 1 | 3 | 4 | 2 | 7 | 9 | 0 | 26 |
| Ujauzito | 0 | 5 | 15 | 25 | 2 | 0 | 0 | 47 |
| Kulawitiwa | 2 | 14 | 34 | 118 | 6 | 1 | 0 | 175 |
| Jaribio la kubakwa na kulawitiwa | 10 | 13 | 15 | 14 | 4 | 0 | 0 | 56 |
| Kukashifiwa | 14 | 37 | 67 | 125 | 9 | 2 | 0 | 254 |

*Kiambatisho Namba 4a:* **IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOAJIRIWA KUANZIA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024**

| No | Kada | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | MFAMASIA | 14 |
| 2 | DAKTARI WA BINAADAMU | 3 |
| 3 | MAABARA | 8 |
| 4 | AFISA MASOKO | 1 |
| 5 | AFISA TABIBU | 18 |
| 6 | AFISA TABIBU KINYA NA MENO | 6 |
| 7 | AFISA TATHIMINI UHIMILI WA MFUKO | 1 |
| 8 | AFISA UHUSIANO | 1 |
| 9 | AFISA USAFIRI | 1 |
| 10 | MFIZIOTHERAPIA | 4 |
| 11 | MUUGUZI MSAIDIZI | 30 |
| 12 | TEHAMA | 4 |
| 13 | SYSTEM DEVELOPA | 4 |
| **JUMLA** | | **95** |

*Kiambatisho Namba 4b:* **IDADI YA WAFANYAKAZI WA KADA ZA AFYA WALIOKUWEKO MASOMONI KWA MWAKA 2023/2024 WA BAJETI**

| NAM | KADA | JUMLA |
|---|---|---|
| 1 | MUUGUZI WA MACHO | 8 |
| 2 | USINGIZI | 13 |
| 3 | DAKTARI MBOBEZI WA MOYO WA WATOTO | 1 |
| 4 | MUUGUZI WA MOYA WA WATOTO | 1 |
| 5 | DAKTARI WA WATOTO | 3 |
| 6 | AFISA USHAURI NASAHA | 6 |
| 7 | DAKTARI WA BINAADAMU | 26 |
| 8 | MAAFISA MAABARA | 16 |
| 9 | MKEMIA | 2 |
| 10 | MADAKRARI MENO | 5 |
| 11 | AFISA LISHE | 4 |
| 12 | UUGUZI | 32 |
| 13 | WAFAMASIA | 13 |
| 14 | AFISA AFYA JAMII | 29 |
| 15 | AFISA MIOZI | 3 |
| 16 | DAKTARI BIGWA WA KUSOMA PICHA ZA MIONZI | 3 |
| 17 | AFISA KUMBUKUMBU NA MAKTABA | 2 |
| 18 | WASAIDIZI AFISA USHAURI NASAHA | 18 |
| 19 | FUNDI SANIFU MADAWA | 3 |
| 20 | DAKTARI WA HUDUMA YA HARAKA | 2 |
| 21 | DAKTARI WA MASHIKIO | 1 |
| 22 | DAKTARI WA BIGWA WA MARADHI YA NDANI | 6 |
| 23 | DAKTAR WA MKOJO | 2 |
| 24 | WAUGUZI WANAONGALIA WAKONJWA KWA UMAKINI ZAIDI (CRITICAL CARE) | 11 |
| 25 | DAKTAR BIGWA WA MACHO | 4 |
| 26 | DAKTARI WA BIGWA WA KINA MAMA | 6 |
| 27 | THEATER MANAGEMENT | 3 |
| 28 | PHYSIOTHERAPY | 3 |
| 29 | DAKTARI MBOBEZI WA PICHA ZA KINA MAMA | 1 |
| 30 | DAKTARI WA MACHO | 2 |
| | **JUMLA KUU** | **229** |

*Kiambatisho Namba 4c:* **IDADI YA WAFANYAKAZI WA KADA ZA AFYA WALIOKUWEKO MASOMONI KWA MWAKA 2023/2024 WA BAJETI**

| NAM | KADA | JUMLA |
|---|---|---|
| 1 | AFISA AFYA WA UTEKELEZAJI | 1 |
| 2 | AFISA AFYA MANUNUZI NA BUGAVI | 2 |
| 3 | AFSA UTUMISHI | 6 |
| 4 | AFISA TEHAMA | 6 |
| 5 | GENDER DEVELOPMENT | 2 |
| 6 | MPANGAJI WA MAENDELEO | 1 |
| 7 | AFISA KUMBUKUMBU NA MAKTABA | 2 |
| 8 | UHUSIANO WA KIMATAIFA | 1 |
| 9 | AFISA MCHUMI | 2 |
| | **JUMLA KUU** | **23** |

***Kiambatisho Namba 5a:*** **TATHMINI YA VITUO VYA AFYA ZANZIBAR MWAKA 2023/2024**

| Wilaya | Dispensary | Health Centre | Total |
|---|---|---|---|
| Chake Chake | 11 | 4 | 15 |
| Mkoani | 11 | 5 | 16 |
| Micheweni | 6 | 6 | 12 |
| Wete | 11 | 6 | 17 |
| Jumla Ndogo - Pemba | 39 | 21 | 60 |
| Kaskazini A | 13 | 5 | 18 |
| Kaskazini B | 6 | 5 | 11 |
| Kati | 15 | 3 | 18 |
| Kusini | 5 | 3 | 8 |
| Magharibi A | 4 | 5 | 9 |
| Magharibi B | 6 | 5 | 11 |
| Mjini | 2 | 5 | 7 |
| Jumla Ndogo - Unguja | 51 | 31 | 82 |
| **GRAND TOTAL** | **90** | **52** | **142** |

## *Kiambatisho Namba 5b:* IDADI YA SHUGHULI JUU YA MASUALA YA JINSIA NA USAWA KWA MAKUNDI YOTE KWENYE JAMII KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

| Programu ndogo | Masuala ya Jinsia Yametambuliwa | Huduma / Matokeo | Bajeti ya 2024/25 '000' |
|---|---|---|---|
| Utawala na Rasilimali Watu | 1. Ukosefu wa madaktari wa kutosha wakiwemo madaktari wa ganzi katika hospitali mbalimbali | Mafunzo ya madaktari wa matibabu na taaluma nyingine za afya ikiwa ni pamoja na madaktari wa geriatric / wauguzi, gynacologists na watoto. | **2,313,046** |
| Afya ya Uzazi ya Mama na Mtoto | 2. Vifo vya juu vya uzazi na watoto wachanga utunzaji mdogo wa ujauzito na ziara ya 4 ya ANC | Kupunguza vifo vya akina mama na watoto wachanga | |
| Afya ya Uzazi | 3. Ufikiaji mdogo wa kupanga uzazi | Upatikanaji wa bidhaa za Upangaji Uzazi katika Vituo vyote vya Afya pamoja na uhamasishaji kwa Wanandoa | **1,003,235** |
| Huduma za NCD | 4. Viwango vya juu vya NCDs ikiwa ni pamoja na kisukari miongoni mwa wazee. | Kuboresha huduma za kliniki kwa wagonjwa wasio na ugonjwa kwa wazee<br><br>Kuongeza ufahamu kwa jamii kuhusu magonjwa yasiyoambukiza na mambo yanayochangia | **120,000** |
| Huduma za HIV/AIDS | 5.Kudhibiti janga la VVU na kuboresha matokeo ya afya kwa PLWHA | Upimaji wa VVU na ushauri nasaha kwa mama wajawazito | |
| Huduma za Matibabu | 6. Ukosefu wa data za kutosha zilizogawanywa juu ya ujazo wa vifaa vya matibabu vya mama na mtoto ikiwa ni pamoja na lishe katika MoH na CMS. | Upatikanaji wa hesabu zilizogawanywa na vifaa vya dawa, vifaa vya vitendanishi. vifaa na chanjo | **18,592,054** |
| **Jumla Kuu** | | | **22,028,335** |

## *Kiambatisho Namba 6a:* MCHANGANUO WA MAOMBI YA FEDHA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2024/2025

| Maelezo | Matumizi ya Maendeleo | | | | Matumizi Mengineyo | | Ruzuku | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mchango wa Serikali | Msaada Washirika wa Maendeleo | Mkopo | Jumla ya fedha za maendeleo | Mshahara | Matumizi ya Kawaida | | |
| **Programu ya Kinga na Elimu ya Afya(PHO301)** | | | | | | | | |
| Huduma za Kinga na Elimu ya Afya | | 863,880,000 | | 863,880,000 | 24,984,784,000 | 9,553,193,000 | | 35,401,857,000 |
| Mradi shirikishi wa Ukimwi,Homa ya Ini,Kifua Kikuu na Ukoma | 380,000,000 | 4,065,000,000 | | 4,445,000,000 | | | | 4,825,000,000 |
| Mradi wa kumaliza Malaria Zanzibar | 645,000,000 | 6,424,000,000 | | 7,069,000,000 | | | | 7,714,000,000 |
| Mradi shirikishi wa Huduma za Afya ya Mama na Mtoto | 1,000,000,000 | 5,194,000,000 | | 6,194,000,000 | | | | 7,194,000,000 |
| Miradi wa Maendeleo | 36,500,000,000 | | 8,984,444,000 | 45,484,444,000 | | | | 45,484,444,000 |
| **Jumla Ndogo** | **38,525,000,000** | **16,546,880,000** | **8,984,444,000** | **64,056,324,000** | **24,984,784,000** | **9,553,193,000** | | **100,619,301,000** |
| **Programu ya Tiba(PHO102)** | | | | | | | | |
| Programu ndogo ya Matibabu(SH0201) | | | | | 24,138,826,000 | 47,640,357,000 | | 71,779,183,000 |
| Programu ndogo ya Uchunguzi(SH0202) | | | | | | | 5,922,200,000 | 5,922,200,000 |
| Miradi ya Maendeleo | 33,975,000,000 | | 30,577,000,000 | 64,552,000,000 | | | | 64,552,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | **33,975,000,000** | **0** | **30,577,000,000** | **64,552,000,000** | **24,138,826,000** | **47,640,357,000** | **5,922,200,000** | **142,253,383,000** |
| **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PH0103)** | | | | | | | | |
| Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH010301) | | | | | 7,564,140,000 | 2,631,089,000 | | 10,195,229,000 |
| Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti (SH010302) | | | | | 1,092,256,000 | 501,200,000 | | 1,593,456,000 |
| Programu ndogo ya Uratibu Pemba (SH010303) | | | | | 24,343,975,200 | 1,181,027,800 | | 25,525,003,000 |
| Programu ndogo ya Tafiti za Afya (SH010304) | | | | | | | 2,070,100,000 | 2,070,100,000 |
| Miradi ya Maendeleo | 500,000,000 | 0 | 0 | 500,000,000 | | | | 500,000,000 |
| **Jumla** | **500,000,000** | **0** | | **500,000,000** | **33,000,371,200** | **4,313,316,800** | **2,070,100,000** | **39,883,788,000** |
| **JUMLA YA FUNGU H01** | **73,000,000,000** | **16,546,880,000** | **39,561,444,000** | **129,108,324,000** | **82,123,981,200** | **61,506,866,800** | | **282,756,472,000** |
| **Hoapital ya Mnazi Mmoja(Fungu HO2)** | | | | | | | | |
| Makadirio ya Kazi za Kawaida | | | | | 23,069,600,000 | 15,260,000,000 | | 38,329,600,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | | | **23,069,600,000** | **15,260,000,000** | | **38,329,600,000** |
| Mradi wa Utanuzi na Ukarabati wa Hospital ya Mnazi Mmoja | 2,000,000,000 | | 21,000,000,000 | 23,000,000,000 | | | | 23,000,000,000 |
| **Jumla ya Fungu H02** | **2,000,000,000** | | **21,000,000,000** | **23,000,000,000** | | | | **23,000,000,000** |
| **JUMLA YA FUNGU HO2** | | | | **23,000,000,000** | **105,193,581,200** | **76,766,866,800** | | **61,329,600,000** |
| **JUMLA YA FUNGU H01 na HO2** | | | | | | | | **344,086,072,000** |

## *Kiambatisho Namba 6b:* MUHTASARI WA MAKUSANYO YA WIZARA YA AFYA 2024/2025

| KIFUNGU | KASMA | MAELEZO | MAKADIRIO YAMAKUSANYO KWA MWKAA 2023/24 |
|---|---|---|---|
| **H0101** | | **Ofisi Kuu Pemba** | |
| | 1421021 | Mapato ya Uchomaji Taka | 20,000,000 |
| | 1422051 | Huduma za Afya ya Wafanyakazi | 90,000,000 |
| | 1422073 | Malipo ya Huduma za Afya kwa wagonjwa wenye BIMA | 50,000,000 |
| | 1423009 | Mapato ya Huduma za Hospitali | 50,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **210,000,000** |
| **H0103** | | **Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali** | |
| | 1422015 | Huduma za Maabara | 750,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **750,000,000** |
| **H0104** | | **Programa ya Kinga na Elimu ya Afya** | |
| | 1421021 | Mapato ya Uchomaji taka | 40,000,000 |
| | 1422035 | Shahada ya Maradhi ya kuambukiza | 600,000,000 |
| | 1422050 | Huduma za Afya Bandarini | 99,700,000 |
| | 1422051 | Huduma za Afya ya Wafanyakazi | 1,000,000,000 |
| | 1422078 | Ukodishwajiwa wa Maeneo ya Kibiashara | 30,000,000 |
| | 1422124 | Mapato ya UVIKO 19 | 99,983,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **1,869,683,000** |
| **HO105** | | **Program ya Tiba (PH0102)** | |
| | 1422073 | Malipo ya Huduma za Afya kwa wagonjwa wenye BIMA | 80,000,000 |
| | 1422095 | Ada ya Usajili wa Tiba Asili | 40,000,000 |
| | 1423008 | Mapato ya Damu Salama | 20,000,000 |
| | 1423009 | Mapato ya Huduma za Hospitali | 60,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **200,000,000** |
| **HO106** | | **Idara ya Uendeshaji na rasilimali watu** | |
| | 1422131 | Ada ya Mafunzo | 20,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **20,000,000** |
| **HO107** | | **Bohari Kuu ya Dawa** | |
| | 1421023 | Mapato ya Hewa Tiba | 30,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **30,000,000** |
| **HO112** | | **Taasisi ya Utafiti wa Afya** | |
| | 1422094 | Mapato ya Utafiti | 50,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **50,000,000** |
| **HO113** | | **Baraza la Wauguzi** | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Wauguzi | 100,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **100,000,000** |
| **HO114** | | **Baraza la Madaktari** | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni Madaktari | 200,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **200,000,000** |
| **H0115** | | **Baraza la Mazingira** | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni wataalamu wa Afya ya Mazingira | 80,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **80,000,000** |
| **H0116** | | **Bodi ya Hospitali Binafsi** | |
| | 1422118 | Usajili na Leseni kwa Huduma Hospitali Binafsi | 130,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **130,000,000** |
| **H0117** | | **Baraza la Wataalamu wa Maabara** | |
| | 1422119 | Usajili na Leseni Wataalamu wa Maabara | 80,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **80,000,000** |
| | **JUMLA KUU KWA FUNGU H01** | | **3,719,683,000** |
| H0201 | | **Kitengo cha Uongozi na Utawala Mnazi Mmoja Hospital** | |
| | 1422078 | Ukodishaji wa Maeneo Kibiashara | 8,200,000 |
| | 1422094 | Mapato ya Utafiti | 400,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **408,200,000** |
| **H0202** | | **Huduma za Uchunguzi na Matibabu** | |
| | 1422073 | Malipo ya Huduma za Afya kwa wagonjwa wenye BIMA | 922,686,000 |
| | 1423003 | Kitengo cha Huduma za Haraka | 8,200,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **930,886,000** |
| | **JUMLA KUU KWA FUNGU H02** | | **1,339,086,000** |
| **JUMLA KUU KWA FUNGU HO1 na H02** | | | **5,058,769,000** |